
JULAI - AGOSTI MMXXVI - TOLEO LA LIII

# NGURUMO
## *ya Mwandishi*




R.I.P
BISHOP
JOHN HILUKA

shajara:

## WARAKA KUTOKA GEREZANI

*yabeba kurasa za mwisho wa Mwandishi*

**HABARI KUU:**

MIAKA 10 YA
TUZO YA KISWAHILI YA SAFAL YA FASIHI YA AFRIKA
Watanzania Watetea Kiswahili Chao, Wang'ara Tena




Picha ya jalada: Hayati Bishop John Hiluka

**HADITHI**
SINDBAD BAHARIA—Uk 15

K.O.K.W.A—Uk 25 & 26

TUHUMA—Uk 27 – 28

**DAWATI LA WATOZI**

+255 766974865 - WHATSAPP

+255 672 160 016 Piga

Richard Mwambe

# YALIYOMO

**MWANDISHI WETU** — Juma Hiza — Uk 3

**PITIO LA VITABU** — DIWANI: CHUNGU TAMU—8 — Uk 5

**SAIKOLOJIA** — Ya Mapenzi/Mahusiano/Ndoa — Uk 5, Uk 6

**MAKALA** — Uandishi wa Kisasa — Uk 7, Uk 8

**KUTOKA KWA FANANI** — Usiyoyajua Kuhusu Kisiwa cha Goree — Uk 9

**SAKO KWA BAKO** — Jonathan Furaha Ngua — Uk 10

**KUTANA NA MWANDISHI** — Hussein Issa Tuwa — Uk 11, Uk 12

**SHAJARA** — Waraka Kutoka Gerezani — Uk 13

**HABARI MOTO** — Miaka 10 ya Tuzo za Safal ya Kiswahili — Uk 16

**SHUBAKA LA VITABU** — Mjue Tawfiq Al Hakim — Uk 17

**KITABU NILICHOSOMA** — MY LIFE MY PURPOSE— 6 — Uk 18

**KUTOKA MAKTABA** — DKT. NDYANAO BALISIDYA — Uk 22

**ELIMU JAMII** — SAFARI YA MALEZI—11 — Uk 23, Uk 24

# MWANDISHI WETU

## JUMA HIZA

**KATIKA toleo letu hili la 53, safu ya MWANDISHI WETU inamleta kwenu Juma Hiza. Ama wengi mwamjua au la, lakini hilo lisiwe kikwazo. Huyu ni mwandishi kijana kabisa, mwandishi wa kisasa tena wa zama zetu. Kwanini mimi nikusimulie wakati yeye mwenye yu hapa? Haya tumsome**

Kama wengi walivyozoea kuniita Juma Hiza na hili ndio jina ambalo nilipewa na wazazi wangu. Huyu Hiza ni baba yangu. Katika familia yetu tumezaliwa watoto watatu, mimi ni mtoto wa pili nikiwa kama kaka. Wa kwanza ni dada yangu anaitwa Jasmine na wa mwisho ambaye ni mdogo wangu anayenifuata anaitwa Mwalimu ila tumezoea kumuita Teacher.

Safari yangu ya uandishi ilianza mapema sana, tangu nilipokuwa Shule ya Msingi Mandela iliyopo Moshi mjini. Nakumbuka nilikuwa napenda sana kuwasimulia wanafunzi wenzangu simulizi za kutunga ambazo wao waliamini ni za kweli. Baadae nikahamia kuziandika kwenye madaftari. Huo ndio ukawa mwanzo. Nilipofika sekondari ikawa ni mwendelezo tu. Ndoto yangu kubwa ilikuwa siku moja kuona *story* yangu ikichapishwa gazetini kama ambavyo nilikuwa naona kipindi hicho mwandishi kama Eric Shigongo, Sultan Tamba na wengineo *story* zao zikichapishwa na kusomwa na wengi.

Niliishi na ndoto hiyo mpaka pale ambapo nilifanikiwa kufika chuo na hapo ndipo nikapata bahati kwa mara ya kwanza *story* yangu kuchapishwa gazetini. Nakumbuka lilikuwa ni gazeti la Uhuru tokea hapo ni kama vile gari liliwaka. Niliamua kuingia rasmi miguu yote kwenye uandishi, nikaipa kisogo taalamu yangu ya uhasibu ambayo iliniweka chuo kwa miaka mitatu. Huyu ndiye mimi Juma Hiza ambaye nimeamua kuufanya uandishi kuwa kazi yangu. Naipenda sana.

Nimejifunza mengi, ila kubwa ni kwamba mafanikio hayaji kwa kutegemea kipaji pekee bali yanahitaji nidhamu, uvumilivu, kujifunza pia kujua wasomaji wanataka nini na muda gani. Siwezi kusema mimi ni bora kuliko wengine ama najua sana ninachokifanya hapana ila wakati mwingine ni Mungu tu. Naamini yeye ndiye anayeendelea kunipa nafasi hii niliyonayo katika uandishi mpaka leo. Sio kwa ujanja wangu, ni yeye.
Mimi nina kitabu kinaitwa CHOZI LISILOFUTIKA ambacho nilikichapa mwaka 2018. Hiki ndio kitabu changu cha kwanza kunitambulisha sokoni na baada ya hapo ukawa ni mwendelezo wa kutoa vitabu vingine kama vile NILISAFIRI NA JINI, USALITI WA MAMA na vingine ambavyo vipo mbioni kutoka. Watu wakae mkao wa kusoma tu.
Lakini nimeandika zaidi ya riyawa 50 mpaka sasa, na kila siku bado naendelea kuandika.

Kiukweli navutiwa na waandishi wengi sana, ukiniambia nimtaje mmoja wengine nitakuwa siwatendei haki. Ila naomba niwataje waandishi watatu tu kwa heshima yao. Wa kwanza kabisa ni Eric Shigongo huyu sio ananivutia tu bali ni Role model wangu, wa pili ni Nyemo Chilongani huyu sio ananivutia tu bali ni amewahi kuwa mwalimu wangu katika Uandishi na watatu ni George Iron Mosenya huyu nae sio kunivutia tu bali namsoma kama darasa, nina mengi ninayojifunza kutoka kwake.
Tukizungumzia soko la vitabu, lina changamoto, hasa kutokana na ushindani mkubwa, mabadiliko ya teknolojia, na tabia za usomaji zinazobadilika. Hata hivyo, naamini ugumu wa soko hauondoi fursa zilizopo. Mwandishi anayezingatia ubora wa kazi, anayejenga uhusiano mzuri na wasomaji wake, na anayetumia ipasavyo majukwaa ya kidijitali ana nafasi nzuri ya kufanikiwa kuliteka soko.
Kwa mtazamo wangu, changamoto zilizopo zinapaswa kuwa motisha ya kuboresha kazi na mbinu za kuifikisha kwa wasomaji, badala ya kuwa sababu ya kukata tamaa. Mafanikio katika uandishi yanahitaji ubunifu, uvumilivu, na kujifunza mbinu mpya za kujitangaza na kuuza kazi zako.
Kwa sasa, kazi zangu zinapatikana kupitia kurasa zangu rasmi za mitandao ya kijamii na kwa mawasiliano ya moja kwa moja. Msomaji anayehitaji kazi zangu anaweza kuwasiliana nami ili kupata maelekezo ya jinsi ya kuzipata, iwe kwa nakala za kidijitali au za kuchapishwa pale zinapopatikana.
Kwa upande wa Instagram napatikana kwa jina la **Jumahizastory**
Kwa upande wa **WhatsApp napatikana kwa namba 0712988278**

Nawapenda sana, bila wasomaji mimi si kitu. Ombi langu kwao wasiache kunifuatilia pia kuniunga mkono.



# KITABU KIPYA MJINI

Mwandishi: Neema Mgao

**GABEDA**
**(MWANAMKE WA DHAHABU)**

Ni riwaya iliyobeba visa na mikasa kumhusu mwanamama GABEDA. Kuanzia kuzaliwa kwake, ukuaji wake, maisha yake ya ndoa, maisha ya utuuzima wake ameona yote aaweke kitabuni.

Yapo mambo mengi mwanadamu hupitia katika maisha yake, ikiwa atapitia mambo mazuri, yatabaki katika kumbukumbu ipendezayo na iletayo raha ndani ya ubongo wa mhusika. Ikiwa atapitia mambo magumu ni wazi kuwa kumbukumbu mbaya zitadumu katika ubongo wake. Atafanyiwa matukio utotoni au atafanyiwa matukio utuuzimani, ubngo una kawaida ya kuhifadhi kumbukumbu hasa zilizo mbaya na ziumizazo ni nadra sana kupotea kichwani.

GABEDA ( MWANAMKE WA DHAHABU) ni riwaya iliyosheheni visa na mikasa ifaayo kwa wazazi na walezi kujifunza kulea watoto wao, vijana kuuishi na kuulinda ujana na usichana wao, na wanandoa kuziishi ndoa zao. Hii ni tiba pia ya kisaikolojia kwa msimuliaji na kwa yeyote ambae amepitia madhila iwe katika ukuaji au katika maisha ya utuuzima.

GABEDA (MWANAMKE WA DHAHABU) karibu kufungua kurasa.

**Kitabu kinapatikana kwa Tsh 15,000** tu katika sehemu zifuatazo.


Dodoma na maeneo jirani— Capital BookStore **0655109158**

Morogoro : Marafiki Bookstore **0719226293**

Makambako: APM Bookstore **0674246969**

Arusha: Kwa Ally Said **0757690302**

Dar es salaam: Kwa George **0755454152**
Mafinga: Konzo Duka la Vitabu **0625646265**
Au wasiliana na mwandishi **0763013206**



# PITIO LA VITABU

## CHUNGU TAMU - 08

DIWANI YA CHUNGU TAMU

MWANDISHI: THEOBALD MVUNGI

WACHAPISHAJI: TPH

MWAKA: 1985

Inatoka toleo lililopita…

**5. NAFASI YA MWANAMKE PAMOJA NA UHURU WAKE KATIKA JAMII.**

**UJUMBE**

v Ni lazima tujitoe mhanga ili kutetea wanyonge

v Dhuluma,unyonyaji,kutowajibika pamoja na uongozi mbaya ni baadhi ya vikwazo vinavyokwamisha ujenzi wa jamii mpya.

v Mashindano ya kutengeneza silaha kwa mataifa makubwa huhatarisha amani duniani.

v Demokrasia ya kweli ndiyo njia pekee ya kuendeleza mfumo wa mageuzi hapa nchini na katika nchi nyingine za ulimwengu wa tatu.

v Mgawanyiko wa watu katika matabaka husababisha kukosekana kwa umoja na mshikamano katika jamii.

v Mapenzi ya dhati yanahitajika katika jamii na ni lazima yadumishwe. Mapenzi ya ulaghai yapigwe vita kwa hali zote.

v Suala la mapenzi na ndoa waachiwe wawili wanaopendana na si maamuzi ya wazazi.

**FALSAFA**

Ø Mwandishi anaamini itikadi itakavyowatetea wanyonge, yenye kuleta haki na usawa kwa kila mtu. Analaani wizi, dhuluma,udikteta,unyonyaji na kila aina ya uovu.Vile vile anatetea uhuru katika mapenzi na ndoa.

**MSIMAMO**

Ø Mwandishi wa diwani hii ana msimamo wa kimapinduzi kwani ameonesha matatizo mbali mbali yanayozikumba jamii zetu na mbinu za kuondokana na matatizo hayo. Miongoni mwa matatizo hayo ni uongozi mbaya, ulanguzi, dhuluma,rushwa,n.k pamoja na namna ya kuyatatua matatizo hayo.


**MUUNDO**

Katika ushairi,muundo ni umbo,ploti pamoja na mjengo wa ushairi.Muundo hupatikana kwa kuangalia idadi ya mistari kwa kila ubeti wa shairi linalohusika.Katika diwani hii msanii ametumia miundo changamano.Miundo mikuu iliyotumiwa na mwandishi ni ;

· Tarbia (mistari minne kwa kila beti) pamoja.Mashairi yaliyotumia muundo wa tarbia ni Chungu Tamu" "Tishio la Binadamu", "Chini ya Mti Mkavu',"Mjanja yu Mashakani" "Radi ya Kiangazi" ,"Shairi la Udongoni,Fikra za Waungwana" ,"Mfereji wa Maringo,) pamoja na lile la "Takukumbuka Daima,')

· Sabilia (mistari mitano na kuendelea kwa kila ubeti).

Mashairi yaliyotumia muundo wa sabilia ni kama vile:- "Daktari Askari","Chanzo ni Wenye Kauli" , "Wimbo Wake Hotubani", "Wengine Wabaki Taabuni", "Ngulu Wapaona, "Chungu na Tamu" "Usiwe Mwnja Asali","Thomas na Doto","Manzese Mpaka Ostabei" pamoja na shairi la "Wosia".Mashairi mengine yaliyobakia yametumia muundo wa tarbia kwa baadhi ya beti na nyingine muundo wa sabilia.




**MTINDO**

Mtindo ni upekee wa mwandishi katika kazi yake.Upekee huo huweza kumtofautisha mwandishi mmoja na mwandishi mwingine. Katika ushairi, kuna aina mbali mbali za mitindo kama vile mtindo unaofuata kanuni za ushairi wa kimapokeo na mtindo unaofuata kanuni za usasa. Mtindo unaofuata kanuni za ushairi wa kimapokeo hutawaliwa na urari wa vina na mizani, muwala, mara nyingi kuna mfanano kwa kila kituo, huweza kuimbika, n.k.

*Itaendelea...*



# SAIKOLOJIA

**Na: NEEMA MGAO**

MALKIA WA SAIKOLOJIA

**+255763013206**

**SAIKOLOJIA YA MAPENZI/MAHUSIANO/ NDOA.**

## JIZUIE KUWA KICHAA KWENYE MAHUSIANO NA NDOA.

Hellow Agosti
Ni mwezi wa nane tumeuanza, Mungu mwema ameendelea kututunuku pumzi yake tusiyoilipia. Mitihani na magumu yapo hayakosekani, jambo la msingi ni kuendelea kuwa imara katika utatuzi wa changamoto mara ikukabilipo.

Katika makala hii ya mwezi Agosti nimeona tuyazungumzie mapenzi, tuyazungumzie mahusiano, tuizungumzie ndoa. Katika mada hii tutazame eneo hili kwa upana sana, na nikukaribishe katika mjadala binafsi kupitia simu namba +255 763 013 206 mijadala iwe kwa njia ya simu au kwa ujumbe whatsapp, ikiwa unalo tatizo hilo na aidha njia nitakazoweka hapa ukaona bado hazitokusaidia, basi karibu nikusaidie.

**KICHAA**
Tafsiri ya neno 'kichaa' ni mtu ambae amepoteza uhimili na utimamu wa akili yake. Kichaa ni mtu ambaye anaweza kufanya jambo la ajabu na yeye akaona yupo sahihi kulingana na upungufu wa akili alionao.

**KICHAA KWENYE MAPENZI/ MAHUSIANO/NDOA.**
Huyu ni mtu ambaye anaweza fanya mambo ya ajabu iwe ya kikatili au yaletayo raha lakini mambo hayo yakafunikwa na mwamvuli wa neno MAPENZI au UPENDO.

Leo ninaongelea mada isemayo JIZUIE KUWA KICHAA KWENYE MAPENZI/MAHUSIANO/ NDOA, ni mada nzuri sana ambayo imani yangu kwayo ni kwamba itakubadilisha au kukuimarisha. Kichaa katika mapenzi inaweza kutafsiriwa kwa maana nyingi, iwe maana iletayo matokeo hasi au matokeo chanya. Matokeo hasi yaweza tokea pale ambapo matendo yakaleta madhara kwa mwingine mfano ukiudhiwa kiasi cha kumpiga na kumjeruhi mwenza wako kutokana na wivu wa kimapenzi. Matokeo chanya ni kama umpendavyo sana mwenza wako kiasi kwamba umemnunulia gari au umepempenda sana na kuchanganywa na mwenza wako kiasi cha kuendelea kuzaa nae na kupokea au kutoa zawadi kwa mwenza wako kila wakati.

**MAMBO YASABABISHAYO KICHAA CHA MAPENZI KUONEKANA.**
Yapo mambo kadhaa ambayo yanaweza kutafsirika kama ni ukichaa wa mapenzi/ndoa.

**A]. KUGOMBANA NA WENGINE KWAAJILI YA MPENZI/MKE/MUME WAKO.**
Mtu mmoja niliwahi kumsaidia kimawazo siku aliyowaza akamchome kisu mwanaume mwingine "aliyesikia" kuwa ana mahusiano na mke wake. Wakati nampa ushauri namna ya kushughulikia uvumi huo kumbe tayari alikua na kisu mfukoni. Mungu mwema alikubali kuwa msikivu na tulipofanya uchunguzi pamoja ikajulikana kuwa siyo kweli ni shutuma za uongo.
Ikiwa unagombana na mwenza wako eti kwasababu tu yupo karibu na watu ambao siyo jinsia yake, wewe ni kichaa, na tiba yake ndiyo hii leo. Kwamba mkeo asicheke na kuzungumza na majirani, mkeo asiende msibani maana atatongozwa, wewe ni kichaa. Eti mumeo akicheka na hao wapangaji wenzenu wa kike, mumeo akifurahi maongezi na hao majirani zenu basi anatembea nao. Tayari unavuta mdomo, unagombana na mwenza wako. Unagombana hata na hao jirani zako, unawaita wenzio malaya kisa wanacheka na mumeo siyo sawa. Na wewe ndiye kichaa ninaekuzungumzia hapa leo.

Utagombana na wangapi? na muda huo maisha ni watu, bila watu maisha hayajakamilishwa bado. Jizuie ukichaa huo, utaumia wewe mwenyewe, utajikuta jamii inakutenga kwaajili ya matendo yako. Kugombana na watu kisa mkeo au mumeo huo ni ukichaa.

**B]. KUMTENDEA UKATILI MWENZA WAKO.**

Wapo watu wameenda mbali zaidi kwa kuwa wanawafanyia ukatili wenza wao kwasababu tu ya maneno ya kusikia. Yupo mtu amekua akimpiga mkewe na kumrukisha kichura chura eti tu kwanini ameonekana akicheka na kutaniana na jirani yake habari za mpira kila Simba na Yanga zinapocheza.

Kumtendea ukatili mwenza wako siyo kwamba ndiyo unamfundisha adabu, hapana, unampa madhara kisaikolojia na utamfanya afanye usaliti kwa kificho na akili kubwa. Bwana mmoja aliniambia kuwa alianza usaliti baada ya mkewe kuwa akimshutumu kuwa na mahusiano na mpangaji mwenzao. Anasema shutuma zilikua kali kiasi akaamua kuanzisha kweli mahusiano maana aliona anasingiziwa bure, bora afanye kweli. Anaendelea kusema kuwa alipomwambia huyo mwanamke aliyesingiziwa nae ilimchukua miezi minne kukubalika kwa mwanamke huyo jambo ambalo hata yeye alilishangaa kwani alidhani kuwa kwakua wan acheka na kuongea na jirani yule alidhani angekubaliwa haraka. Anasema ilikua siku akionekana amecheka na huyo jirani basi na unyumba ananyimwa. Kumnyima unyumba mume wako kwasababu tu amekuudhi, eti kwakuwa anacheka na wanawake wengine, au eti kwakuwa amechelewa kurudi nyumbani basi ndiyo unamnyima unyumba nao huo ni ukatili. ACHA!

**C]. KUJITENDEA UKATILI WEWE MWENYEWE BINAFSI.**

Umemkataza mkeo kujichanganya  na watu, hata misibani hutaki aende eti atatongozwa.
Kila rafiki unaemuona karibu na mumeo humtaki.
Kila rafiki utakaemuona na mkeo humtaki, kwamba mpenzi wako atafundishwa umalaya na uhuni.
Wengine wameenda mbali zaidi, hata akiwa kazini anajipa mawazo kiasi cha kushindwa kula vizuri, kushindwa kufanya kazi vizuri. Mwingine amemshutumu mwenza wake usaliti mpaka akajiua. Kwanini ujitendee ukatili kwasababu tuu umesalitiwa au umeachwa?,. Usijitendee ukatili kwaajili ya mtu ambae mmekutana wote mkiwa watu wazima.

NB:
Natambua wapo watu wanaowafanyia dharau wenza wao huku wakijua fika kuwa hata wao hawatapenda kufanyiwa hivyo. Nasisitiza kuheshimiana zaidi ya yote. Wapenzi, wapendane sana. Mke atambue nafasi yake kwa mumewe, na mume atambue nafasi yake kwa mkewe. Kuheshimiana kuwe nguzo yenu.

JIEPUSHE NA UKICHAA KATIKA MAPENZI NA NDOA, NDOA SI GEREZA KWAMBA NDOTO BINAFSI ZIFE, NDOA IWE MWANZO WA KUZALISHA NDOTO ZA WANANDOA HUSIKA.KILA MMOJA KUISHI NA KUFURAHIA MAISHA INAWEZEKANA. USIOGOPE KUISHI, FURAHI NA WATU, MAISHA NI WATU. KUFURAHI NA WATU SI UHUNI, INGAWA WENGINE WANAWEZA KUVUKA MIPAKA ILA KAMA MWANAMKE AU MWANAUME ANAYEJITAMBUA NA KUPATA HUDUMA ZOTE MUHIMU  NA ZISIZO ZA MUHIMU HAWEZI KUMSALITI MWENZA WAKE . KILA MMOJA ATEKELEZE MAJUKUMU YAKE NA KLUWA MWAMINIFU KWA MWENZA WAKE.

ASANTE.

MADAM NEEMA MGAO.
DODOMA.
TANZANIA.
+255 763 013 206.

**KONA YA RIWAYA BOOKSHOP**

**Tembelea duka letu la vitabu 'KONA YA RIWAYA' Kinondoni Morocco ujipatie vitabu vya riwaya vilivyoandikwa na waandishi mbalimbali wa hapa nchini kwa bei rafiki kabisa.**

**Ulizia kitabu unachotaka, agiza kitabu unachokipenda, nasi tutakutumia kwa uaminifu mkubwa**

**Simu: 0655 428 085**

# UANDISHI WA KISASA NA KILIO CHA SOKO LA VITABU

Na Richard Mwambe

Uandishi wa vitabu hususan vya hadithi na ushairi unakua kwa kasi ya ajabu katika kizazi cha sasa. Kama ilivyo kwa mapinduzi yaliyotokea katika sanaa ya muziki; kutoka ule wa rhumba za enzi zile na kufikia huu wa kizazi kipya, wenye midundo ya kidijitali ndivyo inavyokua kwa upande wa sanaa ya uandishi kwa sasa.

Ukitazama tulikotoka, nyakati zile za 'kina Eddie Ganzel, Hammie Rajab, Ben Mtobwa, Dadi Mwawale na wengine wengi kulinganisha na sasa, zama za 'kina Maundu Mwingizi, Japhet Nyang'oro, Kevin Mponda, Frank Masai, Joseph Shaluwa na wengineo, utaungana nami na kukiri kuwa kuna mapinduzi makubwa sana katika uandishi wa vitabu vya burudani hapa Tanzania. Kama wewe ni msomaji wa tangu enzi za miaka ya themanini au sabini utagundua ladha tofauti sana ya kalamu ile na hii ya sasa. Si tu kwamba kwa sababu kalamu ile ilikuwa ya wino na hii ya dijitali, la hasha! Bali zama zile zilikuwa za analogia na hizi ni za utandawazi.

Kama nilivyobainisha, ukweli ni kwamba uandishi wa sasa ni tofauti sana na ule wa zamani. Kipindi kile—nilichokiita zamani—wigo wa kujua jambo au kupata habari au ufahamu ulikuwa mdogo sana tofauti na sasa. Hili litakupa ushahidi ukitazama ni aina gani ya waandishi waliokuwa wameishika fasihi kipindi hiko. Wengi wao walikuwa waandishi wa habari na wasomi/wahadhiri wakubwa vyuoni. Kwanini kwa waandishi wa habari? Kwa sababu wao walikuwa na muda na zana za kupata habari na kujua matukio mengi sana yanayoendelea ulimwenguni kwa msukumo wa kazi yao. Haingetosha wao kuandika habari tu kuelezea jambo fulani la harakati za ukombozi. Yale mengine ambayo hawakuweza kuyaweka kinagaubaga magazetini kwa sababu ya maadili ya kikazi basi waliyatumbukiza kwenye visa vya kifasihi. Wasomi/wahadhiri wao pia iliwapasa mara nyingi kuonesha umahiri katika kuandika visa mbalimbali ili wanafunzi wapate vitabu vya kujifunzia katika masomo ya Kiswahili na *Litereture*. Baada ya wao sasa ndipo tunakunta kundi tatu ambalo si wanahabari wala wasomi/wahadhiri wa vyuo. Hilo ni la kwanza. Lakini hata wao walikuwa na changamoto nyingi sana tofauti na sisi, kumbuka hakukuwa na kompyuta *(BBC),* hakukuwa na *internet*, hakukuwa na 'usasa' huu tulionao. Iliwapasa kuandika hadithi kwenye madaftari kisha kuipeleka kwa mpiga chapa, halafu ihaririwe (japo kwa wengi kuhariri haikuwa jambo gumu kwa sababu wengi wao walikuwa wnahabari) halafu kutafuta mchapishaji(publisher), naye akuzungushe atakavyo, akunyonye na kukukamua mpaka ubakie kama wale ng'ombe wa—miaka saba ya njaa —waliosimuliwa kwenye kitabu cha Kutoka. Zilikuwa changamoto zao, lakini waliandika.

Naam waliandika, wakauza, na wakapata pesa. Lakini kama ukipata nafasi ya kuongea nao hata leo—kwa wale walio hai—watakwambia shuruba walizozipitia.

**Kuna nini ulimwengu wa leo katika uandishi?** Katika ulimwengu huu tulionao, waandishi wamekuwa wengi sana. Na hii inatokana na urahisi wa upatikanaji wa taarifa. Mtu unaweza ukauzunguka ulimwengu kwa muda mfupi sana, ukatafuta unachotaka kwa muda mfupi sana. Ukirudi kwenye uchapaji, kwa sasa mwandishi si lazima kumtegemea *publisher*, kuna hii 'self publishing'. Zama hizi mwandishi moja kwa moja anatumia kompyuta yake kuandika hadithi au hata simu janja yake. Kila kitu kimekuwa rahisi mno. Na hii imechangia vijana wengi sana kujitambua kuwa wao wanakipaji cha uandishi na kukitumia. Ukienda kwenye meza za wauza magazeti utalakiwa na vitabu vya waandishi vijana, alikadhalika kwenye maduka yanayoeleweka bado utakuta ushindani wa vijana wa kizazi hiki na vijana wa kizazi kile cha wakati ule ambao bado wapo kwenye uga huu wa uandishi.

**Kilio cha Soko la Vitabu:** Tofauti na waandishi wale wa zama zile, hawa wa sasa ukiwauliza changamoto wanazopitia kwenye uandishi, basi wakiorodhesha 'soko' itakuwa namba moja. Soko la vitabu Tanzania limeshuka kwa kiwango kikubwa sana—wanavyodai. Mimi binafsi nimejaribu kufanya uchunguzi mdogo tu wa jambo hili na nimebaini mambo kadhaa ambayo labda yanafanya soko hili la vitabu kuporomoka. Nitachambua moja moja.

**1. Usomaji wa vitabu:** Kushuka kwa ari ya usomaji wa vitabu ninaiweka kama chanzo nambari moja. Miaka ya nyuma ya enzi zile, kumbuka hakukuwa na burudani nyinginyingi kama sasa. Ilikuwa kama si dansi basi ngoma za utamaduni, zaidi ya hapo ni kusoma vitabu na majarida. Hali hiyo ilichangia ari ya usomaji kuwa juu. Mfano mzuri ni mimi mwenyewe, hatukuwa na luninga wala simu, na katika umri ule sikuruhusiwa kwenda dansi au kwenye matamasha

ya ngoma za kiutamaduni hivyo starehe na burudani yangu ilikuwa kusoma kusoma kusoma.

Lakini ulimwengu huu wa sasa mtu ana wigo mpana wa kuchagua burudani atakayo. Mapinduzi haya ya teknolojia yaliyotufanya tuanze kuona maigizo ya sinema yanayofanana kabisa na yale tunayosoma ya katubwetesha kabisa. Tukaweka kitabu kando na kukodoa macho kwenye video na sinema. Na kwa kizazi cha sasa ndiyo kabisa, simu janja imechukua nafasi ya kila kitu katika maisha ya vijana wetu. Watasoma vitabu saa ngapi? Hadithi mnazoandika, tayari mnaziweka kwenye makundi huko *whatsapp* na *facebook* au zinasimuliwa *youtube*, unategemea nani akanunue kitabu chako? Hapa sasa waandishi wa kisasa inabidi kutuliza akili, usizungumzie soko la vitabu ila zungumzia soko la fasihi ili kutuweka sawa katika kile unacholalamika. Soko la vitabu ni kweli limeporomoka lakini si kwa sababu watu hawasomi bali kwa sababu watu hawanunui vitabu.

**2. Uandishi wenyewe wa vitabu:** Katika siku hizi, uandishi umekuwa vululu-vululu. Yaani mtu anachapa kitabu tu aonekane ana kitabu dukani. *Yes!* Ni jambo zuri lakini je; tunafuata taratibu zote za uchapaji wa kitabu, mfano uhariri, uhakiki na grafiksi. Wale wasomaji waliokuwa wanasoma kazi za kina Ben Mtobwa au Hammie Rajab wakishika kitabu cha sasa hukiweka kando baada ya kurasa mbili au tatu tu. Kwa nini? Ataona makosa ya kilugha, makosa ya kisarufi nk. Akifungua cha pili, vivyohivyo, unategemea nini? Ataona waandishi wote za zama hizi hawana umakini na wanachokifanya. Je; ni wangapi wataona hivo? Tunapozungumzia kitabu, hatumaanishi tu yale makaratasi yaliyobanwa pamoja, la hasha! Bali ni mkusanyiko wa mambo mengi. Kitabu ni mkusanyiko wa taaluma mbalimbali, kwanza hadithi yenyewe au shairi lenyewe, pili uhakiki –kuondoa makosa ya kisarufi na mengine madogomadogo, tatu uhariri-hadithi lazima ihaririwe, lugha iwekwe sawa, maudhui, muundo vyote inabidi viwekwe vizuri. Ni kweli kwamba wewe umetunga lakini kuna mtu anajua hicho kitu zaidi yako, nne ni uandaaji wa kitabu chenyewe yaani upangaji wa kurasa na usanifu bora wa jalada, hapa unapaswa kupata mtu mahiri wa *graphics* ambaye ataiona kazi yako kama yake, ataweka maandishi vizuri, atatumia *font* nzuri na mwisho tafuta mchapaji mtulivu. Kuna wachapaji hawana utulivu lazima ujue hilo. Na kabla hujatoka kwa mchapaji hakikisha umekagua na kuridhika na kazi yako.

**3. Fanya uchunguzi:** Kama kuna kitu kinawauzi wasomaji ni kuandika riwaya ambayo mambo yake mengi hayajafanyiwa uchunguzi. Sawa, huu ni uandishi bunifu lakini ubunifu unaingia wapi? Ubunifu ni sanaa ya mtambaji hadithi au mwandishi jinsi anavyosimulia kisa chake, lakini yale anayoyasimulia itapendeza zaidi akiwa na weledi nayo, kwa nini, kwa sababu wengi wa wasomaji wa vitabu wa kisasa wana ufahamu mkubwa sana na hii imesababishwa na utandawazi, nafasi za kielimu kwao n.k. Ukiandika riwaya yako inayohusu ujasusi, basi unapaswa kujua moja mbili tatu za ujasusi, maana yake ni kwamba utapaswa kusoma na kuchunguza medani za kijasusi. Mfano Jasusi mtu wa namna gani, anaishije, anafanyaje kazi zake, jasusi ni nani.

Au ukiandika hadithi ya mapenzi, unapaswa kuyajua mapenzi, mapenzi yana lugha yake, eeh! Fanya mapenzi, elewa hisia ya jinsi tofauti na yako kwenye mapenzi, maumivu yake, visa na mikasa yake. Utapaswa kuuliza, kusikiliza au kufanya kabisa. Mhusika wako ni 'Changudoa' … unamjua changudoa? Ananasaje mawindo yake, anaipataje pesa ya mteja, kwanini amekuwa changudoa. Ikibidi nenda kwa machangudoa ukajifanye mteja uone wanachofanya ujue lugha zao. Ninachotaka kusema na kusisitiza ni uchunguzi wa jambo, walau asilimia ishirini mpaka thelathini za kile unachoandika kiwe sahihi kwa mujibu wa taarifa zinazofikika halafu changanya ubunifu.

**4. Tangaza kitabu:** Sasa umeshachapa kitabu ni kazi ya nani kukitangaza? Ni wewe. Ni wewe kwa kutumia mitandao ya kijamii au njia nyingine yoyote ile ili kuwafikia wasomaji. Hapa sasa ndipo panahitaji uvumilivu na ubunifu. Buni njia za utangazaji ambazo zitamshawishi msomaji kununua kazi yako, usichoke. Hakikisha kila siku umezungumza kuhusu kitabu chako iwe *facebook, instagram* au popote pale. Ikibidi omba mahojiano redioni au hata vituo vya luninga ili uwafikie watu wengi zaidi. Lipia mitandao ya kijamii ili taarifa ya kitabu chako ifike mbali zaidi. Mwisho wa yote tengeneza *connection* mpya kila wakati. Mwandishi umejifungia ndani, huwajui wasomaji wapo wapi. Matukio ya kiuandishi huendi ambapo utakutana na wasomaji wengi na kupata *connection* mpya. Hili nalo tutagusia matoleo yaa mbele.

Ni imani yangu kwamba kama waandishi tukifanya haya yote basi tutamshangaa Mungu kwa jinsi

Wakatabahu!

# KUTOKA KWA FANANI

## Usiyoyajua Kuhusu Kisiwa cha Goree—Dakar

Na:Anna Meleiya Mbise

Jana nilipata fursa ya kutembelea Kisiwa cha Gorée hapa Dakar, Senegal; mahali penye historia nzito ya biashara ya utumwa iliyotikisa ubinadamu kwa karne nyingi. Kisiwa hiki ni ukumbusho wa maumivu, mateso na simulizi za mamilioni ya Waafrika walioondolewa kwa nguvu kutoka kwa familia zao na bara lao. Hapa kama ambavyo niliona kule Benin kuna ule mlango ambao unaitwa *The Door of No Return* yaani ukipita kwenye mlango huo ilikuwa wazi kuwa usingerudi maana ndiyo ushauzwa na kazi ya kutumikishwa ikiisha ungeuwawa na usingerudi kwenu kwa namna yoyote. Ahseee acha tu achaaa!

Niliumizwa sana na simulizi za namna walivyokamata watumwa na jinsi walivyowachambua. Wale walioonekana kuwa na nguvu walichukuliwa kwa ajili ya utumwa, huku wale ambao hawakuonekana kuwa na uwezo wa kutumikishwa wakitupwa baharini.

Wasichana wadogo wenye umri wa miaka kumi na mitatu waliwekwa katika vyumba maalumu kwa ajili ya kuwafurahisha wamiliki wa watumwa, na wale waliopewa mimba walipewa majani fulani ili kutoa mimba hizo, waweze kuendelea kufanya kazi. Na pia wamiliki wa watumwa walichagua wanaume baadhi ambao walionekana kuwa na mvuto na muonekano mzuri hao waliruhusiwa kuzaa na hawa wasichana ila watoto walikuwa mali ya wamiliki wa watumwa na watoto hawa walipokua walisaidia utumwa kwani walifanywa wajione kuwa wao wapo karibu zaidi na wamiliki kuliko watumwa au Waafrika……Ila nyie wazungu waliofanya hii biashara.

Kutembea katika maeneo haya kunakukumbusha thamani ya uhuru, utu na wajibu wetu wa kuhakikisha historia hii haisahauliki kamwe.

Gorée si mahali pa huzuni pekee, bali pia ni darasa la matumaini, mshikamano na uthabiti wa Mwafrika. Linatukumbusha kuwa licha ya majeraha ya historia, Afrika inaendelea kusimama, kujijenga upya na kuandika simulizi mpya zinazojengwa juu ya haki, umoja na utu.

Tuendelee kusimulia historia zetu kwa uaminifu, kujifunza kutoka yaliyopita, na kuwalea watoto wetu katika misingi ya amani, ubinadamu na kujivunia urithi wetu wa Kiafrika.

Pia nilifurahi kutembelea Shule ya Wasichana ya Mariama Bâ, mwandishi Msenegali na nguli ambaye tulisoma kitabu chake 'Barua Ndefu Kama Hii' tukiwa sekondari, je ulikisoma?

Ni kitabu kilichoonesha unyanyasaji wa kijinsia, hasa dhidi ya wanawake na wasichana. Leo nimefurahi kuona Mariama Bâ ameenziwa kwa kuwepo kwa shule maalumu ya wasichana yenye jina lake.

Kaa ukijua kuwa hujui watu warefu walipo mpaka utakapotembelea nchi ya Senegal.

Naripoti nikiwa Dakar, Senegal, na kazi inaendelea. Upo maktaba Anna Mbise Pan-African Mobile Library Tanzania
Anna Meleiya Mbise
21/07/2026



# SAKO KWA BAKO na JONATHAN F. NGUA

**Leo ni sako kwa bako na Jonathan Furaha Ngua kutoka Kilifi, Kenya. Yeye ni mdau wa Kiswahili na msomaji mahiri wa Nguzo ya Mwandishi. Hapa anajieleza juu ya safari yake kupenda vitabu na Lugha ya Kiswahili.**

Mimi ni Jonathan Furaha Ngua kutoka Kilifi, Kenya. Ni mwalimu mhitimu mwenye shahada ya ualimu kutoka Chuo Kikuu cha Mount Kenya. Ni mtafiti wa fasihi simulizi na andishi.

Mara yangu ya kwanza kukutana na kitabu cha Siku Njema mwaka 1998 ndio wakati wa kwanza kupata msukumo na hamasa ya kupenda kusoma vitabu vingi. Ni kitabu ambacho wahusika wake walinitembeza Tanzania kutoka Mwanza mpaka Tanga. Pia wakati nilipokutana na Malkia wa vitabu, Buinda Mjungu, Arusha, Tanzania alizidishia ari ya usomaji wa vitabu.
Vitabu huongeza uwezo wa kufikiri. Pia huongeza unafahamu wa mambo mengi. Vitabu viliniongezea msamiati, maarifa na kuongeza ubunifu.
Katika harakati zangu katika uga wa fasihi nimekutana na wabobezi kadhaa wa lugha ya Kiswahili nchini Kenya, Uganda na Tanzanaia wakiwamo walimu, wanahabari, waandishi na wanaharakati wa lugha ya Kiswahili kama Guru Wallah Bin Wallah, Hayati Ken Walibora, Hayati Charles Hillary, Mrisho Mpoto, Neema Ben Mtobwa, Mwl. Kato Herbert, Mwl. Ndayikengukiye Gordian, Buinda Mjungu, Dkt. Fabiola Fabian Hassan, Profesa Tigiti Sengo,
Aidha nimehudhuria makongamano ya asasi na vyama vya Kiswahili nchini Kenya, Uganda, Zanzibar na Tanzanaia kama Wasta Kituo cha Kiswahili Mufti, Nairobi, CHAKITA, Mombasa, CHAUKIDU, Zanzibar, CHALUFAKITA, Mwanza, CHAWAKITA, Arusha. Warsha, Morogoro na Mombasa, MASIKIDU Kampala Uganda.




Vilevile nimechangia katika majarida ya Kiswahili kama vile Fahari ya Kiswahili, Uganda. Zaidi ya hiyo nimekuwa nikichangia vipindi kadhaa vya Kiswahili katika redio na runinga kama Kumepambazuka, Redio One Sterio, Bahari ya Lugha, Redio Citizen, Ukarabati wa Lugha, KBC, Mwamba wa Lugha, KTN, Nuru ya Lugha, Redio Maisha nk.
Katika utafiti wa lugha hii nimezunguka sehemu mbalimbali zenye vyanzo au asili ya Kiswahili kama Lamu, Pangani, vibambani kwa hayati Sheikh Shaban Robert, Makumbusho, Dar es Salaam,

Mimi nimesoma vitabu vingi vya waandishi wakongwe na chipukizi wa Kiswahili na Kiingereza kama vile Rest in Peace Dear Mother, Hammie Rajab, A coffin from Hong Kong, Hadley Chase, Land without Thunder, Kisasi, Elvis Musiba, Nyongo Mkalia Ini, Rocha M. Chimera, Chura Mcheza Ngoma, Rebecca Nandwa, Kijiji Kisicho na Makaburi, Dickson Mtalaze, Ndege Tunduni, Japhet Nyang'oro, Jitibie Kisaikolojia, Neema Elias Mgao.

Kwa sasa mimi ni naibu mkurugenzi wa elimu katika gatuzi dogo la Magarini, Kaunti ya Kilifi. J.F.N

# KUTANA NA MWANDISHI **Hussein Issa Tuwa**

**HUSSEIN ISSA TUWA, au kama wengi wanavomwita 'Bigwa wa Taharuki' ni mwandishi kijana wa zama zetu, lakini jina lake limepata heshima kubwa ndani na nje ya nchi kupitia simulizi zake tamu na za kusisimua. Katika safu hii tutapita katika safari yake ya uandishi kama yeye mwenye anavyotusimulia**

---

**Kwanza tujuze historia yako ya maisha kwa ufupi (zile struggling za kutafuta maisha)**

Nilizaliwa na kukulia Dar es Salaam. Kiukweli, maisha yangu hayakuwa na simulizi kubwa ya kuhangaika kutafuta maisha; kwani baada ya kuhitimu chuo kikuu nilipata nafasi ya kazi mapema, jambo ambalo namshukuru Mwenyezi Mungu. Hata hivyo, kabla ya hapo, nilipitia changamoto za malezi baada ya wazazi wangu kutengana nikiwa mtoto. Hali hiyo ilinifanya nikue haraka na kubeba majukumu kwa wadogo zangu mapema.

Labda ndiyo sababu sikuwa na muda mwingi wa "kuwa mtoto" kama wengine; nilijikita zaidi katika kusoma vitabu, kuchora katuni na kuandika hadithi. Bila kujua, kumbe huo ndio ukawa mwanzo wa safari yangu ya uandishi.

**Ni jambo lakuvutia sana kujua hilo, na vipi safari yako ya uandishi wa riwaya ilikuwa?**

Safari yangu ya uandishi ilianza kama njia ya kujieleza. Nilipenda kusoma na nilivutiwa na uwezo wa hadithi kuunda dunia mpya ndani ya akili ya msomaji. Baadaye nilianza kuandika simulizi zangu. Hata hivyo, haikuwa rahisi sana kukubalika na magazeti yaliyokuwa yakichapisha riwaya wakati huo.

Kupata uwezo wa kuchapa kitabu changu cha kwanza pia ilikuwa ni changamoto kubwa sana. Hata hivyo, kutokata tamaa na kuamini kile nikifanyacho, kukaniwezesha kupata nafasi ya kuchapishwa: kwanza magazetini na kisha, vitabuni. Leo ninashukuru kuona kazi zangu zimewafikia wasomaji wengi na kuwa sehemu ya safari yao ya kifasihi.

**Upande wa changamoto, ni zipi unapambana nazo katika safari yako ya uandishi na unazivukaje?**

Changamoto kubwa imekuwa ni kudumisha ubora na ubunifu katika kila kazi ninayoandika. Pia changamoto za soko la vitabu, mabadiliko ya teknolojia na kuweka uwiano wa muda kati ya kazi ya ajira, uandishi na kuipa nafasi familia zimekuwa ni sehemu ya kudumu ya maisha yangu mpaka sasa. Hata hivyo, changamoto hizi zimenijenga na zimenifanya niendelee kujifunza, kusoma kazi za wengine, kusikiliza wasomaji na kutokubali kuridhika na mafanikio ya jana.

**Hussein Issa Tuwa ni jina linalotajwatajwa sana kwenye midomo ya wapenda fasihi. Uliwahi kufikiri uandishi ungekuheshimisha namna hii?**

Ni kweli nilikuwa na ndoto ya kuwa mwandishi mzuri, lakini sikuwahi kufikiria ukubwa wa heshima ambayo uandishi ungeleta. Kwangu mimi, heshima kubwa zaidi ni pale msomaji anaponifuata na kuniambia kuwa simulizi yangu imemfurahisha, imemfundisha au imemgusa. Hapo ndipo ninapoona nguvu ya kalamu.

**Kati ya simulizi zako, MKIMBIZI imekuwa maarufu sana. Unafikiri kwa nini?**

Nadhani MKIMBIZI iligusa wasomaji kwa sababu iliunganisha taharuki, hisia na masuala yanayogusa maisha ya kawaida ya binadamu. Pia nilijitahidi kuunda wahusika wenye changamoto na hisia ambazo msomaji anaweza kujiona ndani yake. Lakini ukweli ni kwamba wakati mwingine kazi hupewa maisha yake na wasomaji; mwandishi huandika, lakini wasomaji ndiyo huamua kuifanya iwe sehemu ya maisha yao.

**Mpaka sasa umeshachapa vitabu vingapi? Na ni kipi ukikisoma unasema, "Naam**

**hapa niliandika"?**
Mpaka sasa nimechapisha zaidi ya vitabu kumi na moja. Kiukweli… kila kimoja kina nafasi yake, lakini riwaya ninayoitazama kwa jicho la kipekee ni UTATA WA 9/12. Hii ni kwa sababu niliiandika kwanza kwa ajili yangu mwenyewe. Nilikuwa na msukumo mkubwa wa kusimulia kisa hicho kiasi kwamba hata sikujali sana iwapo wasomaji wangekipenda au kukielewa.
Nilichotaka ni kukamilisha simulizi lililokuwa ndani yangu. Ni kama nilikuwa na maumivu ambayo dawa yake ilikuwa kuandika utata wa 9/12. Hapa kuna somo muhimu pia kwa waandishi wenzangu: Kwamba hufikia wakati, inakuwa sio lazima kwa kazi inayouzwa zaidi ndiyo iwe kazi inayomwakilisha zaidi mwandishi.




**Tueleze ushiriki wa familia yako katika uandishi wako**
Familia yangu ni sehemu muhimu sana ya safari yangu. Uandishi unahitaji muda na wakati mwingine mwandishi unaweza kujikuta umezama sana kwenye dunia ya wahusika wako wa vitabuni ukawasahau wahusika waliomo nyumbani na maishani mwako… lakini nimebahatika kuwa na familia yenye uelewa na msaada. Nimejifunza kuweka uwiano kati ya wajibu wa familia, kazi na mapenzi yangu ya kuandika. Si huwa unaona mara kadhaa huwa nakuja na shemeji yenu, mama yangu, wadogo zangu, kwenye matukio ya vitabu? Napata sapoti nzuri kutoka kwao.

**Waandishi wengi wanaochipukia wanapenda kuwa kama wewe. Unawashauri nini?**
Kwanza nashukuru kwa hilo…ina maana nimeonekana kufaa kuwa kiigizo chema kwao. Ningewaambia kuwa uandishi ni safari ndefu. Wasikimbilie jina kabla ya kujenga uwezo. Wasome sana, waandike sana na wakubali kujifunza kutokana na makosa na kwa wenzao pia. Pia wajijengee nidhamu ya kimaadili. Unajua, mwandishi yeye mwenyewe ndiye chapa yake…yaani, "Brand." Hivyo, wakumbuke kuwa kipaji ni mwanzo tu, lakini nidhamu, uvumilivu na ustaarabu ndivyo vinavyoijenga - au kuibomoa - chapa yake kama mwandishi.

**9. Unaiona vipi kesho ya fasihi Tanzania?**
Nina matumaini makubwa sana nayo. Tanzania ina vipaji vingi na kizazi kipya cha waandishi kina nguvu kubwa. Tunahitaji kuendelea kujenga utamaduni wa kusoma na kusomea uandishi wetu, kulinda haki za waandishi na kutumia teknolojia kufikisha kazi zetu kwa wasomaji wengi zaidi.

*Inaendelea ukurasa wa 24...*

# WARAKA KUTOKA GEREZANI
## *yabeba kurasa za mwisho wa Mwandishi*

PALE jina lake lilipoonekana kwenye luninga kubwa ya The Super Dome, Masaki, sote tulisimama kumpigia makofi na kumshangilia. Bendi ya tarumbeta ya JKT ilimsindikiza kwa ………….. iliyopigwa kwa ustadi mkubwa.
Alikuwa mwenye afya—japo haikuwa njema sana, uso uliojawa tabasamu isiyosimulika kwa maneno. Hundi-ya mfano iliyoonesha tarakimu zilizosomeka 10,000,000 shilingi za Kitanzania ilikabidhiwa mikononi mwake huku Tuzo yenye sura ya Baba wa Taifa nayo ikifuatia pamoja na cheti maalum. Alitangazwa mshindi wa kwanza kwenye tanzu ya riwaya. Nakukabidhiwa tuzo yake na Mgeni rasmi wa siku hiyo …...Huyu alikuwa Bishop John Hiluka.

Bishop John Hiluka aliufunga ukurasa wa maisha yake hapa duniani Mwezi Julai mwaka huu wa 2026. Simanzi, vilio, huzuni zilitawala mioyo na nyuso za wapenzi wa fasihi, waandishi wa hadithi, wasanii wa filamu, ndugu jamaa na marafiki. Katika makaburi ya Chang'ombe, mwili wa MSHINDI huyu wa Tuzo ya Nyerere ya Uandishi Bunifu utanzu wa riwaya katika msimu huu wa nne uliteremshwa kaburini ukisindikizwa kwa nyimbo za maombolezo na maneno yaliyojaa uzito usiopimika "binadamu ni mavumbi na mavumbini utarudi".

Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Fasihi Fund (TAFF) alikuwa mmoja wa waombolezaji. Yeye kama mwandishi anamzungumzia vipi Hayati Bishop John Hiluka?

"Nilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha rafiki yangu na mwenzangu katika tasnia ya uandishi, marehemu Bishop John Hiluka. Kifo chake ni pigo kubwa si kwa familia yake pekee, bali pia kwa tasnia ya fasihi, filamu na sanaa kwa ujumla.
Mimi ni Hussein Msafiri Wamaywa, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mfuko wa Fasihi Tanzania, taasisi inayojihusisha na kuhamasisha fasihi kama nguzo muhimu ya maendeleo na kurejesha utamaduni wa kusoma unaozidi kupotea.
Marehemu Bishop Hiluka alikuwa rafiki yangu wa muda mrefu tangu miaka ya 2005. Tulifanya kazi pamoja katika magazeti mbalimbali; yeye akiwa mchoraji wa vielelezo na mimi nikiwa mwandishi wa hadithi. Mara nyingi nilikuwa naandika hadithi, naye akazipa uhai kupitia michoro yake. Baadaye aligeuka kuwa mhariri mahiri na akanisaidia kuhariri baadhi ya kazi zangu za fasihi.
Kwangu, John Hiluka alikuwa mwanamapinduzi Kindakindaki wa fasihi. Kila tulipokutana, mazungumzo yetu yalikuwa juu ya maendeleo ya fasihi, hasa fasihi ya Kiswahili. Alikuwa na ndoto kubwa ya kuona fasihi yetu inafika mbali na kupata nafasi inayostahili ndani na nje ya nchi.
Nakumbuka mara nyingi alikuwa akiniambia, "Bwana Wamaywa, wewe ni mtunzi mzuri sana." Nilipomjibu kwamba yeye ndiye mtunzi mzuri, alikuwa akitabasamu na kusema, "Hapana, mimi si mtunzi mzuri; mimi ni muendelezaji mzuri. Wewe andika hadithi yako, halafu nipe mimi niikuze." Kauli hiyo inaonyesha unyenyekevu wake na namna alivyothamini kazi za wengine.
Baada ya kupotezana kwa muda kutokana na majukumu mbalimbali, nilimtafuta tena mwaka 2016 baada ya kazi yangu kushinda nafasi ya tatu katika Tuzo za Fasihi za Mabati-Cornell ya Fasihi ya Afrika. Nilitamani aihariri kazi hiyo kabla ya kuiwasilisha kwa matumizi ya kielimu, lakini wakati huo hakuwa na nafasi.
Tulikutana tena mwaka huu kwenye Sherehe za kilele cha Tuzo za Mwalimu Nyerere za uandishi Bunifu mwaka 2025 pale The Super Dome Masaki, ambapo sote tuliingia katika orodha fupi ya washindani kumi bora. Tulipeana moyo na kuzungumza kwa matumaini makubwa kuhusu mustakabali wa fasihi ya Kiswahili. Nilifurahi sana aliposhinda nafasi ya Kwanza katika riwaya kupitia riwaya yake ya Waraka toka Gerezani. Naamini ushindi huo ulikwenda kwa mtu aliyestahili. Tulikubaliana tukutane baadaye ili tuzungumze kuhusu miradi mbalimbali ya kuikuza fasihi, lakini kwa masikitiko makubwa, nafasi hiyo haikuwahi kutokea.
Mbali na mchango wake katika fasihi, John Hiluka alikuwa kiongozi aliyewahi kulitumikia Shirikisho la Filamu Tanzania na alikuwa nguzo muhimu katika sekta ya filamu kama mwandishi wa miswada, mhakiki na mchoraji. Alikuwa mtu aliyependa kuona wengine wakifanikiwa na hakusita kutoa msaada pale alipoweza.
Kwa kweli, tasnia imepoteza hazina kubwa. Hata hivyo, kazi zake, mawazo yake na mchango wake vitaendelea kuishi na kuhamasisha vizazi vijavyo.
Tunamshukuru Mungu kwa maisha yake na tunasema: "Bwana ametoa, na Bwana ametwaa; jina la Bwana lihimidiwe."
Apumzike kwa amani.

# SHAJARA



**Hayati Bishop John Hiluka**

*Hussein Msafiri Wamaywa*
*Mkurugenzi Mtendaji. Tanzania Fasihi Fund - (TAFF) Kisarawe - Pwani.*

Waraka kutoka Gerezani ni riwaya iliyompa ushindi. Mimi na wewe hatujui nini ameandika, hatujui kalamu yake nini imetuambia. Lakini tunaamini jambo moja tu kuwa hii ndiyo imebeba kurasa yake ya mwisho hapa duniani.

Buriani Bishop John Hiluka, kwaheri mwandishi!

***"Safari yangu ya maisha haikuwa ya mstari ulionyooka; ilikuwa ni njia yenye mikunjo, maamuzi magumu, na mwito wa ndani uliokataa kunyamazishwa..."***

Bishop J. Hiluka.

# KUMBUKUMBU YA UPENDO




Ni miaka miwili sasa tangu ulipolala usingizi wa mauti. Ninaendelea kumshukuru Mungu kwa zawadi ya wewe. Mchango wako mkubwa katika kuanzishwa kwa jarida hili bado tunauenzi. Majitoleo yako ya moyo ya kuikuza 'brand' ya Jamvi la Simulizi bado tunayaenzi.

Ulikuwa zawadi, ulikuwa kipaji, ulikuwa mshauri, ulikuwa rafiki, ulikuwa kila kitu kwetu.

Jitihada zako ndani ya Jamvi la Simulizi zimetufikisha hapa tulipo na bado tunaendelea. Tunaamini hata huko uliko bado unasimama na sisi.

Kuondoka kwako hakukutukatisha tamaa bali kulitutia nguvu ya kupambania ulichoanzisha.

Ezenia Stanley Kamana 'Rey Stanley' tunakukumbuka sana, tunakupenda na hatuchoki na hatutachoka kulitaja jina lako.

Endelea kupumzika kwa amani, na sisi tunazidi kukuombea daima.

*"Rest in peace my partiner in crime"*

# SAFARI 7 ZA SINBAD BAHARIA - 03

**Endelea nayo…**
**Eneo lile lilikuwa na madini mengi na makubwa yalokuwa waziwazi. Niliokota almasi na dhahabu kwa wingi pamoja na madini mengine.**

Nilipomaliza nikayafunga kwa uzuri sana na kuanza kutengeneza mpango wa kutoroka pale nilipofungwa. Kwakuwa mapande ya nyama yalokuwa yakitupwa yalikuwa ni makubwa sana, nikachagua lile kubwa zaidi na kujifunga nalo na kujificha kwenye kanzu yangu. Baada ya muda ndege mkubwa sana alikuja ndege aina ya eagle. Ndege yule ana watoto hivyo alichagua pande kubwa na kuondoka nalo. Pande hili ndo lile ambalo nipo. Alinipeleka mpaka kwenye kitundu chake. Na haukupita muda watu wengi wakatokea na kuanza kumtisha ndege yule na kunidondosha mimi na nyama ile.

Kumbe wale wawinda madini kila mmoja alikuwa na kitundu chake, hivyo walishangaa baada ya nyama anatoka na mtu. Niliwasimulia yote yalonipata. Walinipa pole lakini kwa kuwa nilikuwa na madini mengi sana yule mwenye kitundu chake nilimwambia achukue kiasi anachotaka na akachukua pande moja tu. Kisha akaniachia mengine, nikawagawia na wenzie. Tulikaa eneo lile kwa muda wa wiki tukiwinda madini na baada ya hapo tukaanza kurudi baghadadi, kwa kuwa na wale walikuwa wakiishi baghdad ila hatukuwa tukijuana kwa kuwa ni wa mji mwingine.

Njiani tulipita misitu mikubwa na ya kutisha, tulipishana na manyoka wakubwa sana hata tukafika ufukweni na nikauza baadhi ya madini yangu kwenye kisiwa cha Balrora. Nikanunua pale bidhaa kadhaa na zawadi za kupeleka nyumbani. Siku tatu baadae tulipanda jahazi la kuelekea baghadad na tulipofika kwanza nikaanza kutoa sadaka na zaka mali zangu na nikawasimulia ndugu zangu yote yaloniptata.

Walinipongeza sana na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunirudisha salama. Nilikusanya watu na kufanya dua na kutoa sadaka zaidi kama ni shukrani yangu kwa msaada alonipa mwenyezi Mungu hata akanirudisha salama. Niliamua sasa kutofanya biashara nyingine za baharini na kuanza biashara ndogo ndogo. Nilifanya hivi kwa muda wa miezi sita, huku nikawa nafatilia habari za wasafiri. Muda wote huo sikusikia ajali yeyote na walikuwa wakinisifia faida walokuwa wakizipata. Nilivutiwa zaidi na nikasahau machungu yote yalonipata. Nikaamua kuanza safari ingine ya tatau.

Baada ya kumaliza hadithi hii Sinbad wa baharini akampatia Sinbad mbeba mizigo kiasi cha pesa kama ni fidia ya kupoteza muda wake wa kazi na kusikiliza hadithi yake. Kisha akamuahidi kesho awahi ili ajepata yalomkuta safari ya tatu. Akawaambia watu wote walokuwa pale kuwa kesho wawahi maana safari hii amekutwa na mengi ya kustaajabu. Basi watu wote wakatawanyika pale na Sinbad wa baharini akaingia ndani kwake.

## SAFARI YA TATU YA SINBAD

Siku ile ya pili Sinbad mbeba mizigo alivaa nguo zake safi alizonunua na kujipamba vyema na kuelekea kwenye kikao chao. Alipofika alikuta watu wote wamekusanyika tayari wanamsubiri yeye. Alipofika vinywaji viliagizwa na vyakula laini. Watu wakaanza kuburudika, na baada ya muda mzee Sinbad akawasili na kuaza kusimulia safari yake ya tatu kama ifuatavyo:-

Basi niliamua nisafiri tena kwa mara ya tatu, nikafuatilia taarifa za kuwa jahazi linaondoka lini na wapi. Nilikusanya bidhaa za kwenda kuanza nazo na maandalizi nilikamilisha kwa muda wa wiki nzima. Siku ya safari ilipofika ndugu zangu walinisaidia kupeleka mizigo baharini. Walinisaidia na kupandisha pia huku wakinishawishi nisiende. Bila ya kujuwa kitakachonikuta nilikataa ushauri wao na kujitetea kuwa kwa miezi sita sijasikia ajali yoyote iwe leo kisa mimi nimo?

Tulisafiri salama katika visiwa kadhaa na safari ilikuwa ni njema kwakweli. Tulifanya biashara visiwa kadhaa na kuona faida na matunda ya biashara. Hapa nikawa najuta kwa nini sikufanya biashara kwa muda wote huo. Tulikubaliana tuendelee kidogo kufanya biashara kisha turudi nyumbani baada ya siku kadhaa. Ijapokuwa nilipenda tuendelee lakini mawazo ya wengi sikuyakatalia. Basi tukaendelea na visiwa kadhaa hata kukaelekea kwenye kisiwa cha mwisho ili tugeuze. Kwa jumla tulikuwa watu 48 wafanya biashara pamoja na manahodha na wasaidizi tulikuwa jumla ya watu 60.

*Itaendelea toleo lijalo*

www.kitabumarket.co.tz

Na mwandishi wetu.

Kwa namna ya pekee na kupendeza, Tuzo ya Kiswahili ya Safal ya Fasihi ya Afrika imeadhimisha miaka kumi tangu kuanzishwa kwake. Adhimisho hilo lilifanyika katika ukumbi wa Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Sambamba na hilo pia palikuwa na mambo makubwa mawili; mosi ni utoaji wa vyeti kwa washiriki wa semina ya kujenga weledi kwa waandishi wa vitabu yaliyoandaliwa na BAKITA chini ya udhamini wa Safal Kiswahili prize for African Literature na pili ni utoaji tuzo kwa vinara wa uandishi.

Huu ni msimu wa kumi ambapo waandishi wa Tanzania bado wameonesha 'jeuri' kwa kuitangazia dunia kuwa Kiswahili ndiyo chetu. Tuzo hii iliyojichukulia umaarufu ndani na nje ya Afrika imekuwa chagizo kubwa la kuwaibua waandishi vijana wenye vipaji hadimu katika fasihi. Miongozi mwa Watanzania waliowahi kushinda tuzo hii ni Anna Samwel, Enock Maregesi '2015', Hussein Wamaywa '2016', Dotto Rangimoto '2017',Zainab Baharoon na Jackob Ngumbau '2018', Lucas Lubago na Halfan Sudi '2021', Dotto Rangimoto na Salum Makamba '2022' na wengineo wengi.

Tangu kuanzishwa ka tuzo hii Wakenya na Watanzania wamekuwa wakimenyana vikali katika riwaya, ushairi na hadithi fupi.

Katika msimu huu wa kumi, Inspekta Salim Ng'anzi (Tanzania) ametangazwa kuwa mshindi wa kwanza katika utanzu wa riwaya kupitia riwaya yake ya Mwanamkasi Ndio Basi huku Mwl. Mtalaze Dickson (Tanzania) akitangazwa mshindi wa pili kupitia riwaya yake ya Shamba la Mawe. Katika utanzu wa ushairi mshindi wa kwanza alitangazwa Ali Hilal Ali (Tanzania) kupitia diwani yake ya Vizikwa vya Kale huku Lenard Mtesigwa (Tanzania) akiwa mshindi wa pili katika ushairi.

Maina Dominic Dommy kutoka Kenya akatangazwa mshindi wa mkusanyiko wa hadithi fupi.

## MIAKA 10 YA FASIHI
## TUZO YA KISWAHILI YA SAFAL YA FASIHI YA AFRIKA
### Watanzania Watetea Kiswahili Chao, Wang'ara Tena

**Picha ya pamoja ya washindi (walioshika mfano wa hundi) na baadhi ya wageni waliohudhuria hafla hiyo.**



## SHUBAKA LA VITABU

**Bado tunazidi kufungua shubaka la vitabu na kupata hazina kubwa iliyojificha. Kama uliwahi kuisikia Misri ya kale na simulizi zake za kusisimua za mapiramidi na mafarao, basi katika safu hii Mervat Sakr anaendelea kukusimulia kuhusu 'Mapiramidi' ya fasihi kutokaMisri**

Na. Mervat Sakr

### Tawfiq al-Hakim: Mwanzilishi wa Tamthilia ya Kiarabu na Muasisi wa "Tamthilia ya Wazo"

Tawfiq al-Hakim anahesabiwa kuwa mmoja wa nguzo muhimu zaidi za fasihi ya kisasa ya Kiarabu na mmoja wa waanzilishi wa kweli wa sanaa ya tamthilia ya Kiarabu yenye msingi wa fikra na falsafa. Alileta mapinduzi makubwa katika uandishi wa tamthilia kwa kuiondoa katika mipaka ya simulizi na burudani pekee, na kuigeuza kuwa uwanja mpana wa tafakuri na mjadala kuhusu masuala makuu yanayomhusu mwanadamu, wakati, haki na mamlaka. Hakuwa mwandishi wa tamthilia tu, bali alikuwa mwanafalsafa wa fasihi aliyeiona fasihi kama njia ya kuielewa dunia na kuitafakari upya, hivyo akaifanya tamthilia kuwa nafasi ya kuzungumza na akili kabla ya hisia.

**Asili na Malezi:** Tawfiq al-Hakim alizaliwa mwaka 1898 katika mji wa Alexandria nchini Misri. Alikulia katika mazingira yenye mchanganyiko wa tamaduni mbalimbali, jambo lililomjengea tangu utotoni uelewa mpana kuhusu masuala ya jamii na ubinadamu. Alisoma katika miji ya Damanhur, Alexandria, na baadaye Kairo, ambapo alijiunga na Chuo cha Sheria na kuhitimu kama mwanasheria.

Baada ya kuhitimu, alifanya kazi katika Ofisi ya Mashtaka ya Umma katika maeneo ya vijijini nchini Misri. Uzoefu huo ulimpa nafasi ya kushuhudia kwa karibu maisha ya wananchi wa vijijini pamoja na changamoto za mfumo wa haki, urasimu na ufisadi wa kiutawala. Masuala hayo yalijitokeza wazi baadaye katika kazi zake nyingi za fasihi. Baada ya kufanya kazi katika sekta mbalimbali za serikali, ikiwemo elimu na masuala ya kijamii, aliamua kuacha utumishi wa umma na kujitolea kikamilifu kwa fasihi, uamuzi uliobadili kwa kiasi kikubwa historia ya utamaduni wa Kiarabu.


**Mwanzo wa Safari yake ya Kifasihi:** Dalili za mradi wake wa kifasihi zilianza kujitokeza mapema kupitia tamthilia yake ya kwanza, "Al-Dayf al-Thaqil" (Mgeni Mzito), aliyoandika mnamo mwaka 1919. Tamthilia hiyo ilikuwa na ishara za kisiasa zilizokosoa ukoloni wa Waingereza nchini Misri, lakini ilipigwa marufuku kuonyeshwa jukwaani.

Tukio hilo lilidhihirisha mapema uhusiano wa mvutano kati ya fikra na mamlaka katika maisha yake ya kifasihi, na likamfanya aamini kuwa fasihi si chombo cha burudani pekee, bali ni njia ya kueleza mawazo, kuhoji uhalisia wa jamii na kutoa upinzani kwa njia ya alama na ishara.

Tangu hapo, Tawfiq al-Hakim hakujikita katika kusimulia matukio pekee, bali alielekeza juhudi zake katika kuwasilisha wazo lililofichwa ndani ya simulizi, jambo ambalo baadaye likawa alama yake kuu ya kipekee.

**Mwanzilishi wa "Tamthilia ya Wazo":** Jina la Tawfiq al-Hakim linahusishwa moja kwa moja na kile kinachojulikana kama "Tamthilia ya Wazo" (Masraḥ al-Fikra), mtindo wa tamthilia unaojengwa zaidi juu ya mijadala ya kifalsafa na maswali ya kiakili kuliko mfuatano wa matukio au migogoro ya kawaida ya kisanaa.

Katika tamthilia zake, wahusika hubadilika na kuwa vyombo vya kutafakari mawazo, huku jukwaa likigeuka kuwa nafasi ya kujadili masuala ya uwepo wa mwanadamu, haki, mamlaka na maarifa.




*Itaendelea toleo lijalo...*

**UCHAMBUZI WA KITABU CHA RAIS MSTAAFU BENJAMIN MKAPA**

**"MY LIFE, MY PURPOSE"**

**Na PROF. RWEKAZA MUKANDALA**

{Imetolewa kutoka mtandaoni}




Wahuni walitumia uaminifu wake kwa chama kumshawishi akubali. "Ninajisikia kuwa nilitumika na kusalitiwa. Na ukweli ni kwamba mimi binafsi sikufaidika na sikupata chochote". Anasema Mheshimiwa Mkapa.

Kuna kukosolewa kuhusu matumizi ya anwani ya Ikulu wakati mimi na mke wangu tulipochukua mkopo NBC kununua nyumba. Ukweli ni kwamba wakati ule tulikuwa tunaishi Ikulu, tulichukua mkopo kwa mashart ya kawaida ya biashara. Kabla sijaondoka Ikulu, nilimaliza malipo ya mkopo huo na mshahara wangu wa mwisho na mafao yangu, tukapewa hati ya nyumba hiyo. Anasema Mheshimiwa Mkapa.
Kulikuwa pia na swala la RADAR ambayo ilkuwa lazima kuinunua kuimarisha ulinzi lakini manunuzi yaligubikwa na udanganyifu na hatimaye hela zilizolipwa za ziada zilirudishwa kwa Serikali.

Anafikiri ni muhimu kutazama upya suala la umiliki wa uchumi ili watu wengi zaidi wahusike. Kuendelea kushamiri kwa umiliki hasa wa viwanda na mashamba makubwa na makampuni ya Kiasia au Kihindi inaweza ikaleta wivu, na kuleta shida kubwa. Ana wasiwasi na siku za mbeleni kwani umaskini uenda bega kwa bega na uvunjifu wa amani. Lazima tujiulize kama tunajikita katika utulivu na amani.

Anamalizia kwa kutoa ushauri kwa viongozi wa wakati ujao (future).
Onyesha nia na bidii kwa majukumu upewayo.Uwe tayari kuwashirikisha wengine katika mawazo, mafanikio, matatizo na upimaji utekelezaji, consult more.Usifanye kazi kwa kukurupuka na kutotabirikaFuata na tii sheria na taratibuUwe tayari kusikilizaMtafute mlezi (mentor) kama mimi nilivyokuwa na Mwalimu.

Katika sehemu anabainisha umuhimu wa mke wake mama Anna Mkapa. Mapema kabisa katika ukurasa wa 83. Mheshimiwa anampa saluti mama Anna kwamba yeye ndiye gundi iliyo shikilia familia. Anakiri kuwa yeye Mheshimiwa Siyo mtu rahisi kuishi naye na anamshukuru kwa kuwa mtu wa subira na uwezo mkubwa. Amevumilia mengi wakati wa safari za mara kwa mara, kutokuwepo nyumbani mara nyingi na ndiye alibeba mzigo wa kuwalea watoto wao wawili.

**4. KUSTAAFU**
Sehemu ya tatu naya mwisho ya simulizi hii, ni maisha ya mheshimiwa baada ya kustaafu Urais.

Kwanza Mheshimiwa ametumika sana Kimataifa katika nyadhifa na Taasisi mbalimbali ingawa hapendi kusafiri, Taasisi hizo ni pamoja na Club de Madrid The African Wildlife FoundationInvestment Climate Facility for AfricaUN Iniative "Delivering as One"UNCTAD Panel of Environment Persons.UN Commission on the Legal Empowerment of the PoorMwenyekiti wa Seventh Centre tangu 2006Trustee the Aghakhan UniversityThe Mkapa Foundation Kote huku amejichanganya na watu wenye akili nyingi.
Pili, amehusika sana katika upatanisho wa migogoro huko South Sudan, Congo Mashariki, na Kenya.
Mheshimiwa Mkapa, anamalizia simulizi hii kwa kugusia mambo kadhaa.

Kwanza, anaona Rais mstaafu anathaminiwa zaidi uongozi na uwezo wake Kimataifa zaidi kuliko nyumbani, jambo ambalo hata Mwalimu aliliona. Mara nyingi huitwa kwenye hafla ambapo anakuwa kama Ua au pambo ukutani, lakini natakiwa kwenye kazi muhimu na nyeti za kitaifa.Pili, anaongelea umuhimu wa kuanzishwa kwa Baraza dogo kama sehemu ya Bunge kupitia miswada iliyopitishwa na Bunge kabla ya utekelezaji.Tatu, anazungumzia kukosekana kwa itikadi na fikra pevu za kina juu ya mustakabali wa Taifa letu. Inabainishwa kuwa tunahitaji ukombozi wa pili, Kisiasa, Kiuchumi, Kiutamaduni.

Uchambuzi huu umechukuliwa kutoka mtandaoni.

Umefanywa na Profesa Rwekaza Mukandala.

Tulipoona unafaa kusomwa na watu wengi basi tuliona si vibaya kuuweka hapa pia ili na wapenzi wa Ngurumo mjifunze kitu kipya kupitia maisha ya Rais wa awamu ya tatu, Benjamini Wiliam Mkapa.

Aidha kitabu hiki kinapatikana kwenye duka la TPH Bookshop pale Mtaa wa Samora kwa bei rafiki kabisa

Asante na endelea kuwa nasi

# HABARI PICHA
## Matukio ya wanafasihi



Nguli wamekutana! Pichani kushoto ni Hussein Tuwa akibadilishana mawazo na Profesa E. Mbogo



Bakari Mwinshehe Muasisi na Mkurugenzi wa Tungo Tata TV (katikati) akipokea cheti katika Tuzo za Safal



Wanaojua kucheza na kalamu; Maundu Mwingizi mwandishi wa Kitanda cha Kuadi kushoto na Wilbard Makene mwandishi wa Sarafu ya Gavana wakiwa kwenye pozi la kiuandishiuandishi. Picha kama hizi ni hadimu kuzipata.



Dickson Mtalaze akiwa na ngao yake ya ushindi wa pili katika utanzu wa riwaya aliyojishindia kwenye Tuzo za Safal ya Kiswahili ya Fasihi ya Afrika mwaka 2026

**PONGEZI**

**Bodi ya watozi wa Ngurumo ya Mwandishi tunatoapongezi zetu za dhati kwa washindi wa Tuzo ya Safal ya Kiswahili ya Fasihi ya Afrika msimu wa kumi. Salamu hizi zikufikie Salim Ng'anzi, Ali Hilal Ali, Dickson Mtalaze, Lenard Mtesigwa na Dominic Dommy kwa kuibuka kidedea katika tuzo hizi za Kiswahili. Pongezi nyingi sana kwenu!**

## MALENGA WA KILEO

### PENZINI
Na. Hassan Junior Mapenzi

Ndugu yenu ni penzini,
Nimezama kinikini,
Niokoeni jamani,
Nateketea punguani,

Mbona mwaniachani,
Na mwaniona topeni,
Niendako si nilikoni,
Japo ni na wangu wa ubani,

Si ndivyo mnavyozani,
Maaso mwamuasani,
Mwamuweka maswalini,
Takwa lenu li nini,

He! Nanyi mwapasukani,
Wivu mwajaza moyoni,
Kuniona na wangu ayuni,
Kwenu imekuwa nini,

Yu mwangu moyoni,
Kaniganda kiunoni,
Anibeba mgongoni,
nami kanijaa mpaka kichwani,

Kwa kutulia kaeni,
Maisha tuachieni,
Situweke shaurini,
Hatuhitaji zenu hisani,

Bara mpaka Chukwani,
Twabingirisana kisani,
Hayo yatuhusuni,
Mwana wenu yu penzini,

Nimemvika nishani,
Ya penzi maishani,
Simwachi mwezini,
Bali nitamwanika juani,

Mwataka msemeni,
Kama hampo umbeani,
Tuombeeni kwa Manani,
Tudumu na duniani.

Penzini!

## TAHARIRI

Salaam zikufikieni nyote popote mlipo,

Naamini mu salama salimini na mnaendelea vyema na shughuli za kulijenga taifa.
Karibuni sana katika toleo letu hili la hamsini na tatu. Toleo lililosheheni mambo kemkem kama ilivyo ada.

Lakini kwa namna ya pekee limebeba simanzi ya kuondokewa na mwanafasihi mbobevu, mshindi wa Tuzo ya Nyerere ya uandishi Bunifu msimu wa nne, Ndugu Bishop John Hiluka. Safu nzima ya Ngurumo ya Mwandishi tunatoa pole nyingi kwafamilia, ndugu, jamaa na marafiki.

Kifo ni kama safari katika treni; kila mmoja anapanda katika kituo chake na atashuka katika kituo chake. Mwandishi mmoja—simkumbuki jina– aliwahi kusema "mwandishi hafi kwa sababu daima huishi katika maandishi yake".
Pamoja na yote, Bishop ameondoka katika kipindi ambacho alikuwa akisherehekea ushindi mkubwa wa kile alichokuwa akikipigania katika maisha yake. Amepata tuzo, ameenda. Ninachojiuliza, ametuachia wosia gani katika riwaya yake ya "Waraka Kutoka Gerezani"? Maana baada tu ya kurudisha kizibo cha kalamu kwenye kalamu yake, akalala mauti. Fumbo!
Natamani kusoma riwaya hii, natamani kuusoma wosia huu.

Naamini katika riwaya hii ya ushindi atakuwa ame*summarize* vitabu vyake vyote na kutuletea waraka huu kutoka gerezani, gereza la maisha ambapo mwandishi hufungwa kwa fikra tunduizi, maswali yasiyo na majibu, hasira na viongozi na wanasiasa, uchungu kwa jamii yako. Hili ni gereza!

Sikumbuki vizuri maneno aliyosema pale kwenye mimbari siku alipopewa tuzo yake. Lakini nachelea kusema tu kuwa 'alikuwa akituaga, alikuwa akitutakia amani na maisha mema'. Uso wake ulionesha safari, safari ambayo mimi na wewe hatukuijua aghalabu yeye mwenyewe hakuielewa.

Basi, kurasa ya mwisho ya maisha yake ilibeba ujumbe wa 'Waraka Kutoka Gerezani'

Asante!







www.kitabumarket.co.tz






**Falsafa ya uandishi wake**

Falsafa ya uandishi ya Ndyanao Balisidya inaweza kueleweka kwa kuchunguza riwaya zake (hasa Shida) pamoja na makala zake za kitaaluma kuhusu fasihi simulizi, nafasi ya mwanamke, na utamaduni wa Kiswahili. Kazi zake zinaonyesha kuwa aliamini fasihi ni chombo cha kuelimisha, kukosoa jamii na kuhifadhi utamaduni.

Misingi mikuu ya falsafa yake ni:

**1. Fasihi ni kioo cha jamii**



NDYANAO BALISIDYA

1947—1987

Anaonesha kuwa kazi ya mwandishi si kuburudisha pekee, bali kuibua matatizo ya jamii na kuyachambua ili kuchochea mabadiliko.

**2. Uhalisia (Realism)**

Wahusika wake ni watu wa kawaida wanaokabiliwa na changamoto za maisha kama umaskini, migogoro ya kifamilia, elimu, na maadili. Anaandika kuhusu maisha halisi ya Watanzania.

**3. Maadili na uwajibikaji**

Anaamini mwandishi anapaswa kujenga maadili mema na kuonesha matokeo ya maamuzi ya binadamu. Mara nyingi wahusika wanaofanya maovu hukumbana na athari za matendo yao.

**4. Utamaduni wa Kiafrika**

Katika maandishi yake ya kitaaluma alisisitiza umuhimu wa fasihi simulizi, mila na desturi kama msingi wa utambulisho wa jamii ya Kiswahili.


**5. Usawa wa kijinsia**

Alifanya tafiti kuhusu taswira ya mwanamke katika fasihi simulizi na jinsi nafasi za kijinsia zinavyojengwa katika fasihi, akionesha umuhimu wa kuchunguza nafasi ya wanawake kwa mtazamo wa kina.

6. Fasihi kama nyenzo ya elimu

Aliamini fasihi inapaswa kuwafundisha wasomaji kufikiri kwa kina, kuhoji matatizo ya jamii, na kutafuta suluhisho, badala ya kuwa burudani pekee.

Kwa kifupi, falsafa ya uandishi ya Ndyanao Balisidya ni kwamba fasihi ni chombo cha kuelimisha, kukosoa jamii, kulinda utamaduni wa Kiafrika na kujenga maadili kupitia uhalisia wa maisha ya watu. Hii ndiyo sababu kazi zake zimeendelea kutumika katika ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili kwa miaka mingi.



## SAFARI YA MALEZI—11

### 11.0 FAMILIA KAMA SHULE YA KWANZA YA MALEZI

Familia ndiyo taasisi ya kwanza kabisa ambayo mtoto huikuta anapoingia duniani. Kabla hajafika shuleni, kanisani, msikitini au katika jamii pana, mtoto huanza kujifunza maisha ndani ya familia. Hivyo, familia inaweza kuitwa shule ya kwanza ya malezi kwa sababu ndani yake mtoto hujifunza lugha, maadili, tabia, mahusiano, wajibu na namna ya kuishi na watu wengine.

Malezi ya mtoto hayaanzi anapoanza shule, bali huanza tangu anapozaliwa. Kila tendo, neno au mfano anaouona kutoka kwa wazazi na walezi wake humjengea msingi wa maisha yake ya baadaye. Mtoto anayekulia katika mazingira yenye upendo, heshima na uwajibikaji huwa na uwezekano mkubwa wa kukua akiwa mtu mwenye maadili mema na mchango chanya katika jamii.

Katika dunia ya leo, familia nyingi zinakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile mabadiliko ya teknolojia, shughuli nyingi za kiuchumi, migogoro ya kifamilia na kupungua kwa muda wa wazazi kuwa pamoja na watoto wao. Hali hii imeathiri kwa kiasi fulani jukumu la familia kama shule ya kwanza ya malezi. Hata hivyo, licha ya changamoto hizo, familia bado ndiyo msingi mkuu wa malezi bora.

Na. KELVIN JOHN KYARA

0753767930

### 11.1 Maana ya Familia

Tuangalie kwanza maana ya familia, ili tuweze kufahamu umuhimu wake na faida zake. Familia ni kundi la watu wanaounganishwa kwa uhusiano wa damu, ndoa au malezi, wanaoishi pamoja au kushirikiana maisha kwa karibu. Familia ndiyo kitovu cha ukuaji wa mtoto kimwili, kiakili, kihisia na kijamii. Na kama tunavyofahamu umuhimu wa kitovu kwa mtoto kuanzia tumboni kwa mama yake hali kadhalika anapozaliwa, familia ndiyo inayobaki kuwa kitovu chake kikuu, kwa malezi, mahitaji yake nk.

Ndani ya familia, mtoto hupata mahitaji yake ya msingi kama chakula, mavazi, makazi, usalama na upendo. Lakini zaidi ya hayo, hupata nafasi ya kujifunza maadili na tabia zitakazomsaidia katika maisha yake yote.

Kwa Nini Familia ni Shule ya Kwanza ya Malezi?

Mtoto hujifunza lugha kwanza nyumbani: Lugha ya kwanza anayojifunza mtoto hutoka kwa wazazi na watu wa karibu naye. Kupitia mazungumzo ya kila siku, mtoto hujifunza namna ya kuwasiliana, kuuliza maswali na kueleza hisia zake. Vile anavyojifunza ndivyo atakavyovionyesha katika jamii na katika makuzi yake, hivyo kama wazazi na walezi wanapaswa kuwa makini sana katika kumlea mtoto katika hatua hii ya awali.

Mtoto hujifunza maadili ya msingi: Maadili kama ukweli, uaminifu, heshima,ushirikiano na uvumilivu huanza kufundishwa nyumbani. Watoto wengi huiga kile wanachokiona kuliko kile wanachoambiwa. Hivyo wazazi wanapaswa kuwa mfano bora wa maadili wanayotaka kuwaona watoto wao wakiyafuata.

Familia Humjengea Mtoto Hisia za Usalama: Mtoto anayehisi kupendwa na kuthaminiwa huwa na uwezo mkubwa wa kujiamini na kukabiliana na changamoto za maisha. Familia yenye upendo humsaidia mtoto kukua akiwa na afya njema ya akili na hisia. Watoto wengi waliopitia atika familia ambazo walikuwa wananyanyaswa huwa wanakosa kujiamini pindi wanapokuwa wakubwa, hivy familia zinapaswa kuwa makini na aina ya malezi wanayoyatoa.

Familia Humfundisha Uwajibikaji: Kupitia kazi ndogo ndogo za nyumbani, mtoto hujifunza kuwajibika. Anaelewa kuwa kila mwanajamii ana jukumu lake na kwamba mafanikio yanahitaji juhudi na nidhamu. Hivyo kuna umuhimu wa kumfundisha mtoto kufanya kazi hasa zile ndogondogo ambazo zinaendana na umri wake.

### 11.3 Wajibu wa Wazazi Katika Malezi

Wazazi ni walimu wa kwanza wa watoto wao. Wana jukumu la kuhakikisha kuwa watoto wanapata mazingira mazuri ya kujifunza na kukua. Wajibu huu unahusisha:

- Kutoa upendo na matunzo, kusikiliza watoto na kuelewa mahitaji yao, kufundisha maadili mema, kutoa mwongozo na ushauri, kuweka nidhamu kwa njia inayojenga na kuwa mfano mzuri katika maneno na matendo.

Malezi bora hayategemei utajiri wa familia bali yanategemea namna wazazi wanavyoshiriki katika

# ELIMU JAMII

maisha ya watoto wao. Wazazi wanaotenga muda wa kuzungumza na watoto wao hujenga uhusiano imara unaorahisisha malezi.

**10.4 Changamoto Zinazoikabili Familia Katika Malezi**

Katika karne ya sasa, familia nyingi zinakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazoweza kudhoofisha malezi. Miongoni mwa changamoto hizo ni:

- Matumizi makubwa ya simu na mitandao ya kijamii, ukosefu wa muda wa wazazi kutokana na shughuli za kiuchumi, migogoro ya kifamilia, ushawishi mbaya kutoka kwa marafiki na mazingira na kupungua kwa mawasiliano ndani ya familia.

Changamoto hizi zinahitaji wazazi kuwa makini zaidi ili kuhakikisha kuwa watoto wanapata malezi yanayowajenga kuwa watu bora. Wazazi wanapaswa makini sana katika malezi hasa kutoa mud awa kuwasiliana na Watoto wao kujua changamoto wanazopitia, kufahamu marafiki wa mtoto kama ni wazuri au wabaya Pamoja na kuwaongoza katika machaguo mema ya maisha yao ya baadae.

**10.5 Hitimisho**

Familia ni shule ya kwanza na muhimu zaidi katika maisha ya mtoto. Msingi unaowekwa nyumbani huathiri maisha ya mtoto kwa kiwango kikubwa, hata anapokuwa mtu mzima. Wazazi na walezi wanapaswa kutambua thamani ya jukumu lao na kuhakikisha kuwa wanatoa malezi bora yanayojenga maadili, uwajibikaji, heshima na upendo. Jamii bora huanza na familia bora, na familia bora huanza na malezi bora.

SOMA VITABU
- Kwa afya ya ubongo wako
- Kwa kujiongezea maarifa
- Kwa burudani

USISITE
- Kumsimulia mwingine hadithi uliyosoma
- Kumfundisha mwingine yale uliyojifunza
- Kumshauri mwingine kitabu cha kusoma

NI VIZURI
- Kutembelea maktaba
- Maduka ya vitabu
- Kupiga stori na waandishi

## KUTANA NA MWANDISHI


## HUSSEIN ISSA TUWA

*Inatoka ukurasa wa 12*

Kukua kwa Kiswahili duniani kumefungua mwanga mpya na wa ziada kwa fasihi ya Tanzania, kwani hapa ndipo Kiswahili kilipopata pa kupaita nyumbani. Haiwezekani mchele uchambuliwe nyumbani kwetu halafu pilau tukalionje kwa jirani. Kesho ya Fasihi ni tamu sana, lakini tunapaswa kuipalilia vyema hivi sasa.

**Tutegemee nini kutoka kwako? Je, Binti Fundichuma atakuja kwenye nakala ngumu au John Vata atarudi tena?**

Wasomaji wangu waendelee kuwa na matumaini. Miradi hiyo bado ina maisha. Kijakazi Binti Fundichuma ana nafasi ya kuja katika muundo mpana zaidi. Ujaua na huyu naye kuja kwake ni sawa na ule muwasho ulionifanya niilete "Utata wa 9/12." Ana nafasi pendwa sana kwenye miradi yangu ijayo. Ama kuhusu John Vata, milango ya kurejea kwake nilishaifungua kupitia ujio wa "Mkimbizi wa 2," ambayo bado naifanyia kazi taratibu. Kadiri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia afya na muda, kalamu yangu itaendelea kuleta simulizi mpya zenye taharuki, hisia na ujumbe maridhawa.



# K.O.K.W.A—3

***Ilipoishia…***
**Mwili mbichi wa Afrika ulikuwa umelazwa ndani yake huku shingo ikining'inia upande wa pili na kuacha koromeo linalovuja damu nzito. Amata alihisi kama kapigwa shoku ya umeme, aliganda akiwa katoa macho. Wamemleta saa ngapi hapa? Akajiuliza.**

Alipopiga hesabu zake tangu yeye atoke kwenye lile jengo na kumwacha Afrika pale chini mpaka kufika hapo hotelini hakuna kasi ya kibinadamu inayoweza kufanikisha jambo hilo. Akatulia lakini jicho lake bado lilikuwa likiutazama ule mwili. Mbisho wa hodi ukasikika kutoka mlangoni. Akashusha pumzi na kuliacha lile bafu. Haraka haraka akavaa suruali yake na shati. Akauendea mlango na kuufungua. Mbele yake walisimama askari wawili waliovalia nadhifu kabisa pamoja na kijana mmoja aliyevalia sare za wafanyakazi wa hoteli ile.


"Tumepata taarifa kuwa kwenye chumba hiki kumesikika kelele za mwanamke anayeomba msaada.. tunataka kupekua," mmoja wale askari akaeleza. Amata akamtazama yule mfanyakazi aliyekuja na hao askari na kuona kabisa hayuko sawa, wasiwasi na woga vilimtawala.

"Hizo kelele mmesikia saa ngapi?" akawauliza huku akimalizia kufunga vishikizo vya shati lake.

"Hayo siyo maswali ya kuuliza," akajibu yule askari na kumsukumia ndani Amata. Moja kwa moja akauendea mlango wa bafu. Wakati huo, Amata keshachukua vilevikolokolo pale kitandani na kutia kwenye koti lake. Yule askari akamwita mwenzake na yule mfanyakazi ili washuhudie kilichotokea kule bafuni. Kama walikuwa hawajui, basi Amata alisubiri nukta hiyo tu. Alivuta mkoba wake na kutoka. Kabla hajaufunga mlango akatupa chini kichupa kidogo ambacho kwa kupasuka kwake kilitoa moshi mzito. Akafunga mlango na kuchomoa kadi mlangoni.

"Endeleeni na uchunguzi wenu… mnacheza michezo ya kitoto mbele yangu…" akasema huku akiondoka eneo hilo. Akaingia kwenye gari lake na kuyaacha maegesho ya ile hoteli. Akatokomea mjini. Breki yake ya kwanza ilikuwa katika Kliniki ya Masista wa Franciscaine Ankadifotsy. Hakuwa na lolote hapo zaidi ya kuegesha gari na kulitelekeza.

Alivuta hatua mpaka barabara kuu na kutafuta usafiri wa kukodi. Yote hayo ilikuwa ni kutaka kuwapoteza adui zake endapo wangemfuatilia. Taksi ya kwanza akaicha ipite, ya pili vilevile. Ya tatu akaiabiri na kuondoka zake.




"Queen Margret Hotel tafadhali," akamwambia yule dereva. Safari yao ilichukua dakika ishirini na moja tu kufika katika hoteli hiyo ya kizamani iliyojengwa nje kidogo ya Jiji la Antananarivo. Alipokamilisha malipo ya usafiri huo, alivuta hatua ndogo ndogo na kuingia katika hiyo hoteli. Ilikuwa hoteli kubwa yenye hadhi ya nyota nne lakini ilijengwa upya nje ya jengo la zamani lililojengwa na utawala wa Wafaransa kama sehemu ya kupumzikia mtawala. Moja kwa moja alifikia kwenye kaunta kubwa ya mapokezi na kuulizia ni wapi baa ilipo. Alipoelekezwa hakupoteza muda.

Katika baa ile palikuwapo watu wachache sana lakini ukiwaangalia ilitosha kuona ukwasi wa pesa waliokuwa nao. Akavuta kiti na kuketi, punde tu, mhudumu

akamfikia tayari kwa huduma. Alikuwa binti wa kadiri ya miaka ishirini na tano hadi thelathini hivi. Hakuwa mweupe sana wala mweusi sana. Ukimtazama kama ana mchanganyiko wa uarabu na uafrika maana alikuwa na nywele ndevu alizozibana vyema kisogoni pake. Suti aliyovalia ilimkaa kwelikweli, sketi yake fupi iliruhusu miguu minene kuonekana wazi kabisa. Hakuwa mbaya wala mzuri, alikuwa wa kati kati ya hayo mawili.

"Nikuhudumie tafadhali," sauti nyororo ilipenya kwenye ngoma za masikio za kamanda Amata. Akamtazama vizuri kana kwamba hakumuona awali.
"Aaaaah! Nipatie Martin Coctail tafadhali…" akamwambia huku mkono wake ukichukua ile simu ya yule bwana kutoka katika mkoba wake. Yule mhudumu baada ya kupewa maagizo alisimama pale kwa sekunde kadhaa akimtazama kijana huyo shababi. "Haukunisikia?" Amata akauliza kwa upole. Daima kijana huyu pamoja na umachachari wake, hakuwa mkaidi wala mkorofi mbele ya malaika hawa wasio na mabawa.
"No! kichwani pako kuna damu…" akamwambia. Amata akajishika kichwani, na alipoushusha mkono wake akakuta kweli una damu.
"Oh shit! Ipo washroom hapa?" akauliza. Mhudumu yule akamwelekeza na kisha akaenda kuendelea na shughuli yake.
Ndani ya maliwato, amata aliichukua ile simu na kuanza kuipekuapekua. Eneo hasa alilokuwa akilipekua ni kasha la ujumbe mfupi. Kulikuwa na arafa nyingi sana zilizoandikwa kwa Kifaransa na Kiingereza na chache zilikuwa za lugha asili ya Madagaska yaani ki-Malagasy. Hii ndiyo lugha ya taifa hilo yenye asili kutoka familia ya Kiaustronesia hasa tawi la Malayo-Polynesia.

'Kazi yote ameshamaliza Afrika, iliyobaki ni kumuua yeye mwenyewe.
Hakikisha kazi hiyo inakamilika muda uleule tuliyopanga!'

Moja ya ujumbe ulioandikwa kwa Kiingereza chepesi. Amata akashusha pumzi na kupekua arafa nyingine.

'Tuonane usiku huu saa 4:00 Hoteli Concodu, pool side!'

Huu ulikuwa ujumbe mwingine uliomtaka yule mmiliki wa simu ambaye sasa tayari alikuwa marehemu akutane na huyo aliyeandika ujumbe huo. Concodu Hotel! Akawaza na kuirudisha ile simu mfukoni maana hakuona vingine vya maana. Zaid ya hiyo, sasa mkononi pake alikuwa kakamta kadi ya kufungulia mlango. Kadi ile juu iliandikwa A' Hotel. Kumbukumbu zake hazikuwa mbali, aliikumbuka hoteli hii lakini hakukumbuka ni wapi ameiona. Amata akabaki njia panda, wapi aanze? Concodu Hotel ambapo msjhenzi yule alikuwa na miadi au A hoteli ambapo ilionekana ndiyo makazi yake? Akapata ukakasi wa maamuzi. Akarudisha ile kadi mfukoni na kutazama saa yake. Ilikuwa saa tatu usiku na dakika zake kumi na mbili. Alikuwa na dakika arobaini na nane tu ili awe pale Concodu Hotel. Aliusukuma mlango wa maliwato na kurejea kwenye kiti chake. Alipoketi tu, yule mhudumu akafika na bilauri moja kwenye chano chake. Akaitua na kumuwekea kinywaji mezani. Jicho la binti yule likatua tena kichwani pa Amata. Bado ile damu ilikuwapo maana hata alioingia kule washroom alisahau kilichompeleka na kuanza kufanya vitu vingine. Amata akajishika tena kichwani.

"Pole una mambo mengi sana," yule mhudumu akamwambia Amata. "Tongasoa hisotro!" akamwambia akimaanisha 'karibu kinywaji' kisha yeye akaondoka. Wnawake wenye upendo hivi wapo wachache sana! Akawaza na kuanza kunywa taratibu. Dakika kumi na tano baadae, tayari alikuwa ameshamaliza. Bili yake ilipofika akalipa bila ubishi na kumwachia yule mhudumu tip ya dola 10. Akaondoka zake. Nje ya hotel ile akaabiri taksi jingine na kumtaka dereva kumpeleka Concodu Hotel. Yule dereva badala ya kuondoa gari, kwanza akamtazama mteja wake.
"Umesema Concodu Hotel?" akauliza.
"Ndiyo, mbona unaniuliza?" Amata akajibu na kumtwanga swali.
"Aaaa… hapana! Utalipia Ariary 25,000 tu," yule dereva akamwambia Amata. Hata hivyo Amata alijua kuwa lipo jambo, kwanini dereva yule amwangalie kwa mshtuko namna ile?
"Sina Ariary kwa sasa… nina dola tu!" akamjibu yule dereva.
"Sawa! Dola tano tu za Kimarekani," akatamka huku akiwasha gari na kuondoka zake.

**Soma riwaya hii kupitia**

**www.kitabumarket.co.tz**

# HADITHI: TUHUMA (1)- Na: Shujaa Maneno

**SURA YA I**

INSPEKTA Kombo aliegemeza vyema bunduki yake ya Sub Machine Gun kwenye jiwe lililo kando yake. Kitako cha bunduki hiyo kiligusa ardhi huku mtutuwake ukiwa kimya kwenye lile jabali. Akainua mkono wake na kutaama saa yake ya mkononi. Alikuwa na sekunde thelathini za kutumia kulenga shabaha yake.

Akaichukua darubini yake na kuiweka machoni pake. Alipohakikisha anachokiona ndicho, akaiacha darubini ile ining'inie kifuani pake. Akaichukua ile bunduki na kuelekeza mtutu polepole upande wa lile korongo, akiiweka shabaha yake kwenye kona kali ya barabara iliyochongwa kwenye mteremko mkali wa vilima vinavyotazama mji wa Kyela.

Inspekta Kombo alichagua mahali hususa pa kufanyia shambulio hilo. Alipoiseti vizuri ile bunduki kwa pigo hilo, akaweka alama mahala pale; kisha akashusha bunduki hiyo na kuanza kufanya marekebisho madogo kwenye pedi ya kitako chake.

Chini ya eneo lake la kimkakati alilolichagua kwa uangalifu, Kombo aliona kwamba taa za Kyela mjini zilikuwa tayari zinamulika-mulika katika giza la jioni lililokuwa likiingia. Msafara wa magari uliokuwa ukitoka Dar es salaam ulionekana kama kwa mbali kwa taa zake zilizokuwa zikiwaka kwenyemagari hayo. vilionekana vidogo sana kutoka alipo na vilipo.

Inspekta huyo aligundua kuwa hakuna gari hata moja lililochepuka kwenye njia panda iliyoko chini ya mlima ule ambayo ingemfanya kupoteza lengo lake. Alifikiri na alijua kuwa ni madereva wachache sana ambao wangejihatarisha kwa hiari kupita njia hiyo ya mkato ya mlimani baada pindi tu giza likiingia. Akatikisa kichwa juu chini kuafikiana na uamuzi waliofuanya madereva wale.

Hii ndiyo ilikuwa njia ya haraka zaidi na ya utulivu zaidi ya kuvuka kuelekea Mpaka wa Malawi na Tanzania, na ilikuwa barabara ambayo Sesko Kavilondo angetumia kufika huko.

Akiwa ameridhika na maandalizi yake, Inspeta Kombo alilaza mgongo wake kwenye mwamba mkubwa na kuijaribu silaha yake iliyotiwa mafuta vizuri. Kila kitu kilikuwa tayari, na alikuwa na wakati. Na sasa angeweza kumsubiri Sesko.

Akiwa amezingirwa na giza lililokuwa likiongezeka, Inspekta Kombo alipitia kichwani mwake shughuli za mtu huyo anayemsubiri.

Biashara ya Sesko ilikuwa vifaa vya kielektroniki, ambavyo kwa kawaida vilinunuliwa kupitia kampuni feki,yaani kampuni isiyokuwapo. Lakini ukweli ni kwamba vifaa hivyo vilikuwa vya wizi kutoka maeneo mbalimbali na hasa katika ofisi za serikali. Kisha alisafirisha vifaa hivi vya teknolojia ya juu kwa siri kutoka Tanzania kuingia Malawi na nchi nyinginezo, na kutoka huko viliuzwa Afrika Kusini, Angola na nchi nyinginezo kwa kutumia nyaraka za kughushi, kisha kusambazwa maeneo mbalimbali.

Meli za mizigo kwenye Bahari za Indi na Atlantiki zilibeba mizigo hiyo ya thamani katika hatua ya mwisho kutoka nchi za Afrika na kupeleka kwingineko. Sesko Kavilondo alikuwa ameanzisha njia hii ya usafirishaji na kuishi maisha mazuri kwa faida ya biashara yake haramu.

Shughuli zake za hizo hatimaye zilikuwa zimevuta umakini na hisia za idara ya usalama wa taifa TISS na jeshi la Polisi. Hata hivyo, Inspekta Kombo alikuwa ni tishio zaidi kwa usalama wa Sesko. Inspekta Maulid Kombo alikuwa mpelelezi machachari sana katika jeshi la polisi kitengo cha CID ambaye alikuwa ametatua kila kesi ya ujasusi wa kiviwanda aliyoishughulikia na nyinginezo nyingi ambazo vigogo waserikali wamekuwa wakihusika. Ametishiwa kuuawamara kadhaa, achilia mbali kuwekewasumu vyakulani lakini badala ya kuacha na hayo ndiyokwanza aliongeza bidii hata kama hakutumwa na mkuu wake. Maulid Kombo alikuwa akimfuatilia Sesko kwa karibu sana. *Kwanini mtu huyu atiwi nguvuni? Nyuma yake kuna nani?* Ndilo swalialilokuwa akijiuliza. Hata alipopeleka shauri hilo kwa mkuu wake alipewa ahadi hewa na kisha lilitupiliwa mbali.

Kwakuwa alikuwa akizungukwa na vigogo kwakutoa bakshishi iliyonona, Sesko aliona hakuna wa kumsumbua ijapokuwa jina la Maulid Kombo lilimnyima usingizi.

Ndiyo, mfanyabishara huyo haramu alikuwa mzuri sana katika kile alichokifanya. Alikuwa mtaalamu sana. Kiukweli Inspekta Kombo na ile bunduki yenye ufanisi usio na hisia ya SMG ndiyo walistahili kuumana na mtu huyu. Linapokuja suala la kuangamiza, SMG haikua nahuruma hata kidogo.

* * *

USO WA SESKO KAVILONDO ULIKUNJUKA na kuwa tabasamu jembamba huku akijipongeza kwa mpangilio wake mzuri wa muda. Alikuwa amechagua wakati sahihi wa kuondoka. Maajenti wa serikali walikuwa wamekwama kwenye urasimu mikononi mwa mtu huyu. Na Inspekta Kombo alikuwa bado akifuatilia kila kidokezo kwa utaratibu huko Mbeya. Alichagua Mbeya kwa sababu alishapata fununu kuwa mshenzi huyu atapita huko. Siri ya mafanikio ya Sesko hadi sasa ilikuwa ni kuwa hatua moja mbele kila


wakati. Alijua kila mpango wa kiusalamadhidi yakelakini alichofanya ni kuununua
Alipofika kwenye ile njia panda kabla ya kuuanza mlima Kyela, alikata kona na gari lake la Mercedes kuelekea kushoto kupanda barabara ya kuupanda mlima huo kisha akaangalia muda kwenye saa ya dashibodi ya gari hilo la kifahari la Kijerumani. Dakika hamsini bado zilibaki kabla ya kufika mpakani. Angefika akiwa bado ana muda wa ziada.
Sesko alikuwa amewatumikia vyema mabwana zake wa Kizungu. Hakukuwa na namna ambayo wangemnyima hifadhi kwa sasa kama ingebidi, hasa si kwa nyaraka alizobeba kwenye mkoba wake wa ngozi: mipango ya mchakato sambamba (parallel processor) ya Supercyber 3000. Michoro ya mtandao huu tata wa mifumo ya kimoduli ingemtosha sana kumlinda dhidi ya hatari yoyote. Ndani ya wizi wake huo mulikuwa na mpango nyeti na wa siri. Hazikuibiwa tu kompyutakama unavojua wewe bali hasa kile kilichomo ndani ya kompyta hizo na vifaa vyake. Haukuwa wizi kama wizi unavyodhani wewe, bali ni lile swala la kusema tunaondoa vifaa hivi na kuweka vipya, hivyo vya zamanivinapigwa mnada hewana Sesko angenunua vyote kwa bei ya kipumbavu, lakini vigogo walilofanya hilo walijua kinachoendelea haikuuzwa kompyuta bali uliuzwa mfumo, ziliuzwa taarifa.

* * *

INSPEKTA KOMBO ALIHIFADHI DARUBINI YAKE na kuchukua nafasi yake ya kufyatua risasi. Lile Mercedes la rangi nyeusi lilionekana kama gari la farasi wa kichawi kwa jinsi lililopauka kupitia darubini (scope) ya bunduki yake.
Kombo alisikia mabadiliko ya mlio wa injini wakati dereva alipopunguza gia akitoka kwenye kona, kisha akakanyaga mafuta na kuliharakisha gari hilo kupanda mwinuko unaofuata.
Kombo alilenga alilenga mbele kidogo ya shabaha na kufinya kifyatulia risasi.
Tairi la mbele la kulia likachanika na kupasuka vipande vipande.
Hakukuwa na muda kwa Sesko kudhibiti tena gari pale lilipoteleza kuelekea ukingo wa barabara usio na kizuizi cha usalama. Lile Mercedes liliteleza upande mmoja kuvuka ukingo wa jabali. Mshenzi huyo alinaswa nyuma ya usukani, akipiga kelele huku gari likiporomoka kwenda chini kabisa hadi lilipogonga mwamba uliojitokeza.
Gari lililipuka na kuwa dhoruba kubwa ya moto wa miale mieupe na buluu moshi mweusi na mzito wa mafuta, vioo vilivyovunjika vipande vipande, na idadi kubwa ya mabaki ya vyuma vilivyosambaratika na kujipinda.

Inspekta Kombo alitazama bila kuonyesha hisia zozote huku lile gari lililokuwa likiungua likidunda tena kwenye ukuta wa mwamba na kuanguka kwa kelele kwenye mawe yaliyomomonyoka chini yake. Sasa Sesko Kavilondo alikuwa jambazi mwingine mzembe ambaye amekuwa sehemu ya takwimu za vifo vya Maulid Kombo.
Inspekta huyo kijana, akiwa ndani ya sare yake ya kipolisi aliachia tabasamu pana kwa lile alilolifanya. Akashusha bunduki yake nakuitua ardhini kisha mkono wake ukachomoa pakiti ya sigara na kutoa moja kisha kuibana kwa papi za midomo yake. Aliporudisha pakiti mfukoni, akachukua kiberiti cha gesi na kuiwasha. Alipiga pafu tatu za haraka na kisha akaichomoa na kuibana kwa vidole vyake akitazama kule ambako Sesko alitumbukia na gari lake…

***Nini kitaendelea? Usikose sehemu ya pili katika toleo lijalo.***



# KALAMU YANGU

## GARASA—Laura Pettie

Leo tunaitazama kalamu ya Laura Pettie katika hadithi ya Garasa. Kumbuka Garasa ndiyo ilimpa ushindi wa Tuzo Nyerere msimu wa tatu Bi. Laura (72). Ndugu msomaji, ni wakati wako kujua nasi Ngurumo tunakujuza kinagaubaga. Hata kama hakupenda, tulihakikisha anazungumza...

**Bibiye Laura hebu kwanza tuambie, tangu umetangazwa Mshindi wa kwanza kwenye kinyang'anyiro Cha TUZO Nyerere msimu ule wa Tatu mpaka Sasa... Unajisikiaje?**

JIBU: Huwa naamini tuzo ni alama ya heshima, kwamba kazi yako imetambulika na kuheshimishwa. Ni jambo la kujivunia kwa mwandishi yeyote popote. Ni jambo linaloleta raha na ari ya kuendelea kuandika. Nimekuwa nikipokea meseji kutoka kwa walimu wa shule mbalimbali za sekondari za serikali ambapo nakala za riwaya ya GARASA zimesambazwa. Mirejesho yao baada ya kuisoma inaleta faraja mno. Naweza kusema, najisikia furaha kuwa sehemu ya historia ya tuzo hii. Lakini pia kwa upande mwingine, ni jambo linalonifanya nizingatie sana kujifunza zaidi kila kukicha.

**Hebu tugeukie kazi Yako hii iliyokufanya ung'are... GARASA. Mtanzania akisikia GARASA moja kwa moja anakumbuka mchezo wa karata wa albastini... Vipi kwenye riwaya hii umezungumzia mchezo wa karata au ni kitu Gani hasa?**

JIBU: Hapana, sijauzungumzia mchezo wa karata kama ulivyo. Isipokuwa, maudhui yaliyomo ndiyo yamesadifu maana ya neno GARASA.

**Kama sivyo, je Kuna uhusiano Gani Katika simulizi yako na mchezo huu wa karata mpaka kufikia GARASA?**

JIBU: Pengine nianze na maana ya neno GARASA. Katika mchezo wa karata, GARASA ni ile karata ambayo haina thamani. Lakini papohapo, karata hii ni lazima iwepo mchezoni ili mchezo mzima uchezeke. Hivyo, ni haina thamani ila ni muhimu mchezoni. Msomaji anayeisoma riwaya ya GARASA, pale anapofika mwisho ndipo anapogundua namna ambavyo binadamu wanaweza kuwa GARASA, kwenye mchezo wa kuzichanga karata za maisha.

**Mambo matamu kwelikweli... Laura, Kila shabiki wako na wapenzi wa fasihi Kwa ujumla wanatamani kusoma GARASA. Hebu tupe matumaini kitabu kinakuja?**

JIBU: Sina la kusema, nakiri kuiona kiu yao ya kunisoma na ninaiheshimu sana sana sana. Kitabu lazima kije. Ni miaka 7 tangu niingize kazi mpya sokoni. Kwa namna ambavyo Kiroba kimetamba miaka yote hii bila kufifia, nina hakika GARASA itakuja kusimama pembeni ya Kiroba ikiwa kama kazi bora kabisa.

**Baada ya kusoma kitabu Cha KIROBA CHEUSI - Kwa bahati mbaya sijasoma kile Cha DIRA YA MOYO - nimebaki na swali ambalo wengi linawasumbua; ni vipi unapata mikasa hii?**

JIBU: Mikasa mingi ya kwenye vitabu vyangu, aghalabu huwa inatoka kwenye mawazo yangu. Wakati mwingine naweza kuliona tukio sehemu, hata barabarani tu, halafu baadaye tukio hilo likanijia tena kichwani, na papo hapo nikaanza kuuwaza na kuuona kichwani mwendelezo wa tukio lenyewe. Na wala halihitaji kuwa tukio kubwa sana. Inategemea tu ni kwa kiasi gani limefanikiwa kuivuta nadhari yangu. Wakati mwingine, naweza kujiwa na mazungumzo fulani kichwani, na huo uka-

wa mwanzo wa kipande fulani cha simulizi ndani ya hadithi husika. Wakati mwingine, ni katika kusoma na kutafiti kuhusu jambo fulani, basi naweza kupata wazo la kutunga mkasa juu ya jambo hilo. Mimi ni *Pantser,* kwa hiyo katika kuandika, mkasa mmoja unaweza kuzaa mikasa mingine kadiri ninavyotiririka.

**Wakati unawasilisha muswada wako pale TUZO Nyerere... Hukuhofia anwani hii ya GARASA inaweza kukuangusha?**

JIBU: Kibinadamu kuna hofu fulani ndogo inakuwepo kwa kujua ushindani ni mkubwa na kazi nyingi zina ubora. Lakini pia, niliwasilisha kazi niliyoamini imejitosheleza vyema. Binafsi niliipenda GARASA si kama mwandishi, bali kama msomaji namba moja wa kazi zangu mwenyewe.

**Sasa Laura huyoooooo anapaa, atasomwa mashuleni na kwingineko... Lakini je kalamu yako inapokelewaje na familia Yako?**

JIBU: Inapokelewa vyema sana. Nina familia ambayo inanisoma, na inaniunga mkono katika hatua zangu zote za uandishi na changamoto zake. Wakati fulani, baba yangu, Mzee Kissakwa, aliulizwa swali na mtu, huyu Laura Pettie Kissakwa wa kwenye GARASA ni binti yako? Katika utu uzima huu, baba aliponisimulia hili na namna alivyofurahi kulijibu swali hilo, nilitokwa machozi ya furaha. Nina matumaini hata wajukuu na vitukuu wataipokea kalamu yangu kwa heshima kubwa.

**Laura wewe ni mwanamke mzuri, mwenye haiba nzuri kiasi kwamba huko mitandaoni vijana wanapigana kumbo kimya kimya, kila mmoja anatamani azame nawe kwenye shumbi la mahusiano.... Hebu nambie, unafikiri hili ndilo linakuletea wapenzi wengi kwenye kazi zako?**

JIBU: Hahahahaaaa naweza kusema HAPANA!! Naamini wapenzi wasomaji wangu wanavutiwa zaidi na kazi ninayofanya. Kuna wasomaji ambao walianza kuvutiwa nami hata kabla ya kujua aliyeandika hicho kilichowavutia ni mwanamke. Na ndiyo maana kuna baadhi yao walianza kwa kuniita kaka, mkuu, bro', hata ile kunishtua na kauli kama oyaa we jamaa nk. Mpaka pale walipokuja kugundua Laura ni mwanamke.

Sikatai kuwa huenda wapo wanaovutiwa na Laura kama mwanamke, lakini siamini kama ndiyo kitu ambacho kinawaweka karibu. Dunia ina wanawake wengi warembo mno na wanazaliwa wengine kila kukicha, binafsi ninatamani zaidi nitazamwe kwanza kama mwandishi, niwavutie kwanza kwa maandishi, nikizungumziwa iwe juu ya umahiri katika uandishi, hayo mengine yawe ziada tu ya kibinadamu ambayo kwa kawaida inaweza kubadilika, ikaenda na kupotea. Vinginevyo, kama ninavutia kwa kiasi hicho basi utukufu ni wake Mungu.

Jamani mmemsikia Laura? Mmeielewa kalamu yake kwenye Garasa? Kama una lolote la kumuuliza basi tuandikie whatsapp **0766974865**



## Tangazo




www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi
kila baada ya miezi miwili